SUPA JACKPOT
TZS. 1,117,417,539
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Afariki** dunia kwa kujirusha toka ghorofani

UKURASA 3


HOTUBA

Jumatano Mei 24, 2023 Nipashe 11

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI MHE. PROF MAKAME MNYAA MBARAWA (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

UKURASA 11

Nipashe
Jumatano Mei 24, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581320
www.ippmedia.com
The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Rais Samia akerwa rushwa Mahakama

• **Aibua** 'madudu' katika hukumu... *Endelea ukurasa wa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi mbalimbali baada ya kuwaapisha majaji sita wa Mahakama ya Rufani na Mwenyekiti wa Baraza la Maadili nchini, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Marekebisho ya sheria yalivyoleta mageuzi katika sekta madini

UKURASA 3



Picha tofauti zikimwonyesha Wakili Baraka Mkama akiwa amedhibitiwa na askari polisi, Mbaraka Liyonjo, baada ya kudaiwa kuzuia askari kuwakamata wateja wake walioachiwa huru na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam jana. **PICHA: KULWA MZEE**

## Wakili azua purukushani kortini akizuia wateja wake kukamatwa

UKURASA 2

**MICHEZO** **NABI ANASA FAILI LA WAARABU** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Samia akerwa na rushwa mahakamani

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameinyooshea kidole mahakama kuhusu rushwa inayotumika kwenye kesi za wafugaji na kukwamisha utoaji wa haki.

Aidha, ametaka majaji wanapoondolewa kwa sababu ambazo si za kiafya, apewe taarifa badala ya kupewa taarifa za kuteua kuongeza idadi.

Samia aliyasema hayo jana Ikulu Chamwino baada ya kuwaapisha majaji wa Mahakama ya Rufani huku akisema watendaji wa mahakama za chini wanatakiwa kuangaliwa kwa jicho la kipekee kutokana na kuendelea kufanya mambo ya ovyo.

"Huko chini bado mambo yanaendelea ovyo ovyo. Tumesikia kesi ya Lindi wafugaji wamefanya makosa ya waziwazi wamekamatwa kwenye makosa, Jaji akasema nakwenda huko huko kutazama na kurudi akasema hawana makosa. Sasa utajiuliza kuna nini hapo.

"Sasa hiyo kesi moja ya Lindi, Mkuu wa Mkoa akasema sikubali niambiwe nakiuka maamuzi ya mahakama lakini sikubali hili ni kosa. Sasa inaleta mgongano kati ya vyombo viwili vya serikali. Hilo ni moja, hatujui mangapi huko chini lakini ukisikiliza kesi za wanaoingia kwenye hifadhi huko TANAPA (Shirika la Hifadhi za Taifa) wapi zikifika mahakamani mmmh mambo magumu kidogo," alisema.

Fedha za wafugaji, alisema zinafanya kazi kwa kiasi kikubwa na kuhitajika kutupiwa jicho zaidi ili wananchi wa kawaida wapate haki zao.

"Mama wa Baraza la Maadili, ni imani yangu kuwa una uzoefu na utakwenda kuliongoza vyema baraza hili. Sisi sote tunawatazama ninyi. Jaji (Sivangilwa) Mwangesi lakini akishafanya yake analeta huko kwenu. Kwa hiyo tunatarajia tutakwenda kuongeza kasi katika kujenga maadili ndani ya serikali," alisema.

Rais alihimiza kuongeza kasi ya kujenga maadili ya viongozi na utumishi wa umma bila kumwangalia mtu usoni.

"Kama Baraza lako la Maadili lipo upande upande, tuletee sema huyu hanifai nibadilishie. Tutabadilisha ili uwe na watu waliowenyooka, ili mumwongoze Jaji Mwangesi naye afanye kazi yake vizuri," alisema.

Rais Samia aliwataka majaji walioapishwa kuzingatia viapo vyao vya kufanya kazi bila upendeleo, huba wala chuki.

"Bahati mbaya majaji wakiingia tunafanya sherehe, tunawapaisha lakini wakitolewa kwa ile bahati mbaya hatusikii nani katolewa kwa bahati mbaya, ila naletewa huyu kwa bahati mbaya amepata maradhi tunaomba tuongezewe huyo. Wale wa bahati mbaya stara huko kwenu ipo kubwa ya kustiri hamtaki waadhirike.

"Lakini tungependa kujua kina nani wanaondoka kwa bahati mbaya. Sina wasiwasi kwa ngazi za juu huku Jaji Mkuu jicho lako linafanya kazi kubwa kwa karibu zaidi. Kule Mahakama za chini zinahitaji jicho zaidi," alisema.

Samia alisema amedhamiria kufakikisha kunakuwapo na usawa wa kijinsia kwa Majaji wa Mahakama ya Rufani ambao kwa sasa uwiano wao ni 47 kwa 50.

"Kwa hiyo kila nikitengeneza jopo nitaleta na wanawake ili nifikie 50 kwa 50 jambo ambalo hatukulizoea huko nyuma. Kwa sasa, kwa sababu wapo wana sifa na nina hakika majaji wanawake ni wazuri zaidi huwa wanaogopa dhambi zaidi," alisema.

Naye Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema Watanzania wanatarajia kuona ongezeko la kazi kwenye utendaji wa majaji hao.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alimpongeza Rais kwa kuendelea na safari ya kuhakikisha kunakuwapo na usawa wa kijinsia kwenye uteuzi wa nafasi mbalimbali za uongozi na ngazi za uamuzi.

Awali, Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alisema idadi ya majaji wa Mahakama ya Rufani kwa sasa wamefikia 31, hivyo majopo ya majaji hayo yamefikia tisa na kupunguza mzigo wa mashauri.

"Kwa wastani hadi Aprili 30, mwaka huu, kulikuwa na mashauri 5,636 ambayo yalikuwa yamesajiliwa Mahakama ya Rufani na ukiyagawa katika haya majopo, kila jopo lina uwezo wa kushughulikia mashauri 33. Utaona kwamba mzigo kabla ya majaji sita ulikuwa 805 lakini baada ya kupatikana hawa, mzigo utashuka hadi 626," alisema.

Alisema pia uwepo wao utasaidia kupunguza mrundikano iwapo shauri lililosajiliwa litachukua miezi 24.

"Majopo yanapoongezeka muda wa kukamilisha mashuari unakuwa mfupi na wananchi wanapata haki kwa haraka, kwa hiyo sisi tunaona ni faida kubwa sana kutokana na ongezeko la majaji," alisema.

Jaji Mkuu alisema mashauri yanayohusu benki na kodi ni kikwazo kwa mahakama huku akibainisha kuwa kwa sasa kuna zaidi ya mashauri 200 yanayohusu benki.

"Hayo ni mashauri mengi sana yameshikilia fedha nyingi za biashara na uwekezaji. Bahati mbaya utaratibu tulio nao ni wa kila mtu kukimbilia mahakamani badala ya kutumia utaratibu wa kutatua migogoro kwa usuluhishi ambao ungepunguza mashauri mengi ya benki.

"Mashauri 52 kuhusu kodi haya yanashikilia biashara na uwekezaji pia. Kama tungetatua kwa njia mbadala, hizi fedha zingeweza kurudi kwenye mzunguko na kufanya kazi," alisema.

***• Imeandikwa na Augusta Njoji, DODOMA, na Christina Mwakangale, DAR.***



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akitia saini katika kitabu maalum maarufu kama 'Golden Book', baada ya kuwasili Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Sharm El Sheikh nchini Misri kuhudhuria mkutano wa Mwaka wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) jana. Wa (pili kushoto) ni Rais wa Benki hiyo, Dk. Akinwumi Adesina. **PICHA: OMR**

# Purukushani zazuka mahakamani

**Na Kulwa Mzee**

PURUKUSHANI za vuta nikuvute zimeibuka kati ya polisi na Wakili wa Kujitegemea, Baraka Mkama, katika viwanja vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu baada ya wakili huyo kuzuia askari kuwakamata wateja wake.

Vurugu hizo ziliibuka jana baada ya mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Romuli Mbuya kuwaachia huru washtakiwa watatu waliokuwa wanakabiliwa na mashtaka ya kughushi stika za dawa mbalimbali, wakionyesha ni halisi wakati si kweli.

Hakimu Mbuya alifikia uamuzi huo wa kuwaachia chini ya kifungu cha Sheria Na. 225 baada ya upande wa utetezi kupinga maombi ya Jamhuri ya kuahirisha shauri hilo.

Wakiwa mahakamani, Wakili wa Serikali, Faraji Nguka, aliifahamisha mahakama kwamba upande wa Jamhuri una shahidi mmoja lakini mtunza vielelezo ana udhuru. Ameshindwa kufika mahakamani. Wakaomba shauri lisikilizwe leo.

Wakili wa Utetezi, Agatha Fabian, alipinga maombi ya Jamhuri, akaomba mahakama iliondoe shauri hilo mahakamani kwa kuwa ni la muda mrefu.

Mahakama baada ya kusikiliza hoja, ilikubali maombi ya Wakili wa Utetezi na kuwaachia huru washtakiwa chini ya kifungu Na. 225 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Baada ya kutolewa kwa uamuzi huo, washtakiwa Khalid Somole na Betty Mwankikusye walitoka mahakamani wakikimbia kwa lengo la kukwepa kukamatwa tena.

Washtakiwa wengine ambao hawakukimbia ni Raphael Lyimo na Abdiel Mshana.

Wakati watuhumiwa hao wakitaka kutoweka katika viunga vya mahakama, askari waliwazingira wakitaka kuwakamata, hapo ndipo Wakili Baraka Mkama alipoingilia na kutaka kuzuia hatua hiyo.

Walivutana kuanzia eneo la mapokezi hadi katika lango kuu la kutoka mahakamani. Wakili Mkama alifanikiwa kumsukuma askari Mbaraka Liyonjo getini.

Purukushani hizo zilimpa nafasi Betty ya kukimbia lakini askari walifanikiwa kumkamata Khalid pamoja na Wakili Mkama na kuwaweka mahabusu kwa muda kisha waliwapeleka Kituo Kikuu cha Polisi kwa hatua zaidi.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa wanadaiwa kula njama ya kutenda kosa la kughushi kati Machi Mosi na Machi 31, 2019.

Katika shtaka la pili, wanadaiwa kuwa Machi 18, 2019, katika Mtaa wa Amani na Simba jijini Dar es Salaam, wakiwa na nia ovu, walighushi stika za dawa mbalimbali wakionyesha hazijapita muda wa kutumika na zimetolewa na Keko Pharmaceutical Industry (1997) LTD huku wakijua si kweli.

**JICHO KISHERIA**

Wakili Frank Chacha, akizungumzia purukushani hizo, alisema wateja wao wengi wanaachiwa na kukamatwa.

Alisema mteja anaweza kukamatwa. Wakili anapaswa kutulia na kusubiri utaratibu utakaofuata lakini haiwezekani kuingilia na kuzuia askari kufanya kazi yao.

"Kitendo cha wakili kuzuia askari wasikamate wateja wake ni kosa. Hivyo, kushikiliwa na polisi ni sawa.

Wakili akifanya hivyo, wanamkamata tu. Ni kosa hakutakiwa kuwazuia askari kufanya kazi yao," alifanunua Wakili Chacha.

## Rais Samia amteua Katibu Mkuu wa UVCCM kuwa DC

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amemteua Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Kenani Kihongosi (pichani) kuwa Mkuu wa Wilaya ya Urambo mkoani Tabora.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, Kenani anachukua nafasi ya Said Mtanda aliyeteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara.

Taarifa hiyo ya Ikulu ilibainisha kuwa Mtanda anachukua nafasi ya Meja Jenerali Suleiman Mungiya Mzee atakayepangiwa majukumu mengine.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Rais Samia amemhamisha kituo cha kazi Queen Sendiga kwenda kuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, akitokea mkoani Rukwa.

Makongoro Nyerere aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, amehamishiwa Mkoa wa Rukwa, akichukua nafasi ya Queen.

"Mabadiliko, uhamisho na uteuzi huu unaanza mara moja. Uapisho wa Mkuu wa Mkoa mpya utafanyika kesho (leo) saa 10:00 jioni," ilibainishwa katika taarifa hiyo ya Ikulu.

Zuhura hakuweka wazi sababu za kufanywa kwa mabadiliko hayo kwa viongozi hao wa chama na serikali.



# CHADEMA yasikitishwa kushuka bei ya pamba

**Na Alex Sayi,** SIMIYU

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) mkoani Simiyu kimesikitishwa na kushuka kwa bei ya pamba kutoka Sh. 1,800 na 2040 kwa msimu uliopita 2022 mpaka Sh. 1,060 kwa kilo, hali inayoendelea kuwadumaza wakulima wa zao hilo.

Akizungmza wakati wa uzinduzi wa mikutano ya hadhara kimkoa, Mwenyekiti wa Taifa wa Baraza la Vijana la CHADEMA (BAVICHA), John Pambalu, alisema katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, wakulima wa pamba wanaendelea kutokutendewa haki na serikali kutokana na kushushwa kwa bei ya zao hilo licha ya gharama za maisha kuwa juu.

"Nakumbuka bei ya pamba mwaka jana ilikuwa Sh. 2,040 na leo bei elekezi wanasema Sh.1,060. Imekuwaje bei ishuke kiasi hicho? Hii inaonyesha namna Chama Cha Mapinduzi (CCM) na serikali yake isivyowajali wananchi wake," alisema.

Pia alisema kuna haja kwa serikali kupitia upya upangaji wa bei za nafaka nchini kwa kulinganisha na kupanda kwa maisha ya wananchi wake ili wanapouza, wamudu maisha yao na kuwafanya wakulima waendelee kuona kilimo kweli ni uti wa mgongo.

Licha ya kuzungumzia hili, Pambalu alisema CHADEMA inaendelea na kampeni ya kuhakikisha kuwa Tanzania inapata Katiba Mpya na Tume Huru ya Uchaguzi, ili CCM isibweteke na iwe na nidhamu kwa Watanzania.

Katibu Mkuu wa BAVICHA, Twaha Mwaipaya, alisema anamshukuru Rais (Samia Suluhu Hassan) kwa kuruhusu mikutano ya hadhara ili kila chama kinadi sera zake kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwakani na uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Simiyu, Mussa Onesmo, aliwaomba wananchi mkoani hapa kurudisha imani kwa vyama vya upinzani ili viwatumikie tofauti na ilivyo sasa wabunge na madiwani wa CCM wameshindwa kuwashirikisha na kuwatetea hususani katika suala la kupanda kwa bidhaa na kushuka kwa bei ya pamba ambayo ni tegemeo kwa wakulima.

Onesmo aliongeza kuwa Baraza la Diwani limeazimia kujenga halmashauri mpya maeneo ya Ng'hami itakayogharimu Sh. bilioni moja bila kuwashirikisha wananchi kwa kuwa madiwani hao, mbunge na baadhi ya wakuu wa idara wamejitwalia maeneo Ng'hami na wametegeshea fidia.

Naye Sylvester Kasulumbai, aliyewahi kuwa Mbunge wa Maswa Mashariki kwa tiketi ya CHADEMA, alisema wananchi katika wilaya hiyo wameendelea kuonewa bila kuwa na utetezi wa madiwani na wabunge.

KONGAMANO UWEKEZAJI KATIKA MADINI

# Marekebisho sheria yaleta mapinduzi sekta ya madini

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imekusanya Sh. bilioni 650 kutokana na mirabaha ya sekta ya madini mwaka huu wa fedha (2022/23), kukishuhudiwa mageuzi mkubwa kulinganisha na Sh. bilioni 168 zilizokusanywa katika sekta mwaka 2018 wakati ambao marekebisho ya sheria za madini yalikuwa hayajafanywa.

Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam katika hafla ya uzinduzi wa Kongamano la Uwekezaji katika Sekta ya Madini la Mwaka 2023 lililopangwa kufanyika jijini Oktoba 25-26 mwaka huu.

Dk. Biteko alibainisha kuwa tayari sekta imechangia zaidi ya Sh. trilioni moja katika mapato ya nchi mwaka huu wa fedha huku asilimia 40 ya mapato ikitoka kwa wachimbaji wadogo.

"Ushiriki wa serikali katika shughuli za uchimbaji madini umesaidia kutatua changamoto za kodi zilizokuwa zinaikabili sekta. Pia umekuza ushiriki wa wachimbaji wadogo ambao sasa wanachangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Biteko, wizara inalenga kukusanya mrabaha wa Sh. bilioni 800 katika mwaka ujao wa fedha. Inalenga kuinua mchango wa sekta katika Pato la Taifa hadi kufikia asilimia 10 ifikapo 2025, mwaka ambao ni ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999 hadi 2025.

Waziri huyo alisema hivi sasa wachimbaji wadogo wamechangamka kulinganishwa na utendaji wao wa awali na mchango wao ni mkubwa katika sekta ya madini, ingawa wengi wao wako nyuma katika kusaidia miradi ya kijamii.

"Kwa sasa wanachangia takriban asilimia 40 ya mapato ya biashara ya madini. Hii inachangiwa na ushirikiano mzuri kati ya wawekezaji wa kigeni ambao wanatoa msaada wa kiufundi kwa wachimbaji wadogo kama inavyotakiwa na Sheria ya Madini," alieleza.

Kongamano hilo litawaleta pamoja wadau wakuu takriban 2,000 kutoka sekta ya madini, maofisa wa serikali, wawekezaji na wataalamu wabobezi katika sekta hiyo ili kutafuta fursa, kukuza ushirikiano na kuonyeshana njia kwa ajili ya maendeleo na uchimbaji endelevu wa madini.

Pia litatumika kutangaza utajiri wa rasilimali za madini ya Tanzania na kutoa fursa kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuja na miradi mikubwa ya madini, kutangaza mafanikio ya Tanzania katika sekta ya madini na kutoa fursa ya miradi ya kuongeza thamani ya madini ya aina mbalimbali.

Waziri huyo alisema kongamano hilo linatarajiwa kuongeza kasi ya ushirikiano na ukuaji wa uhusiano kati ya wadau katika sekta ya madini na hivyo kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi kupitia sekta ya madini.

Kongamano hilo limeandaliwa na DMG na Ocean Business Partners (OBP) kwa ushirikiano na Serikali ya Tanzania na washirika wengine wa sekta ya madini, likiratajiwa pia kutumika kuchochea ongezeko la watalii nchini.

Abdulsmad Abdulrahim, Mkurugenzi wa Kampuni ya Ocean Business Partners Tanzania LTD na mwandaaji wa kongamano hilo, alisema mkutano huo utawakutanisha wawekezaji wanaotafuta fursa katika sekta ya madini.



Mwalimu wa Shule Kuu ya Sayansi Akua na Teknolojia ya Uvuvi, Ditran Nagiro (kulia), akitoa maelezo kuhusu kipimo cha kujua idadi ya samaki walioko kwenye maji kwa wanafunzi waliofika kwenye maadhimisho ya nane Wiki ya Utafiti na Ubunifu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Afariki dunia baada ya kujirusha toka ghorofani

**Na Maulid Mmbaga**

MTU mmoja aliyetambulika kwa jina la Joel Misesemo maarufu kama MC Joe kwa mujibu wa mtandao anaoutumia wa Instragram, anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 30 na 35, amefariki dunia baada ya kujirusha kutoka ghorofa ya saba katika jengo la Derm lililoko Makumbusho, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, mmoja wa walinzi katika jengo hilo ambaye hakutaka jina lake litajwe, alisema tukio hilo lilitokea jana saa 11:00 alfajiri.

Alisema kijana huyo alikuwa na utaratibu wa kufika katika jengo hilo mara kwa mara na jana alipofika, alipaki gari lake aina ya Suzuki lenye namba za usajili T 142 DRM na kupanda hadi ghorofa ya saba na kujirusha kupitia dirishani.

"Kamera ya CCTV inaonyesha kuwa alipofika aliingia kwenye lifti alipofika ghorofa ya saba, alitoka na kwenda kupanda dirishani akatanguliza miguu kichwa kikafuata akajiachia akadondoka chini na kupasuka, jinsi inavyoonekana alidhamiria kujiua," alisema.

"Alikuja vizuri na kupaki gari lake na nyuma ya lile gari kuna begi jeusi na mfuko mweusi ameliacha. Ukiliangalia begi kwa makini lina nguo ndani na nimeona kuna wallet kaiweka kwenye begi na chupa ya maji. Bado hatujafahamu kwa nini kaamua kukatisha uhai wake," aliongeza.

Pia alisema askari polisi walifika eneo la tukio na kuuchukua mwili wa kijana huyo na kwenda kuuhifadhi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mwananyamala.

Mmoja wa mashuhuda waliokuwapo eneo la tukio, Christopher Albert, alisema kijana huyo anaonekana ni mwenyeji wa eneo hilo na kwamba saa 11:00 alfajiri wakati watu wakiwa wanaswali, alifika katika jengo hilo na baada ya dakika tano walisikia kishindo na walipopogea kuangalia walikuta mtu amelala chini.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Jumanne Muliro, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, akisema uchunguzi unafanyika ili kujua sababu za kijana huyo kujiua.

Mmoja wa marafiki zake aliyeandika kwenye mtandao wa Instagram, Kelvin Kibenje, alisema alikuwa kijana mwenye ndoto kubwa, alijitolea sana kwenye mambo mengi hasa matukio ya kijamii na kidini.

"Nakumbuka aliniambia alivyokuwa anampenda mke wake, leo kamuacha peke yake. Wanaume tunapitia mengi, lakini tufikie hatua ya kujitoa uhai," alisema.



Mwonekano wa sehemu ya nyumba za wafanyakazi wa Kiwanda cha Nguo Urafiki, Dar es Salaam, ambazo zinatumika kama ofisi, pembeni ni kontena la kuhifadhia bidhaa na kulia ni gari likishusha bidhaa kwa ajili ya kuweka kwenye ofisi mpya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasiwasi watanda bodi iliyofanya uamuzi Urafiki

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA sehemu ya pili ya ripoti hii jana, tuliona mkakati mpya wa kuondoa wafanyakazi 200, kutokutimizwa ahadi ya Waziri Mkuu na kilio cha stahiki za wafanyakazi. Endelea...

Wafanyakazi wanaonyesha wasiwasi kuhusu kuwapo bodi. Wanasema kikao cha Bodi ya Kampuni kilifanyika Agosti mwaka jana na sasa wanapewa taarifa ya maelekezo ya bodi kwamba waliamua wafanyakazi wote waondolewe.

"Kwanini wamechukua muda mrefu sana kutufikishia taarifa? Kuna nini kimeendelea? Meneja Mkuu wa kiwanda hiki ambaye ni raia wa China aliondoka mwaka 2015, hatujawahi kuambiwa kwamba kuna Meneja Mkuu mwingine. Mtanzania tuliyekuwa tunamwona anatekeleza majukumu ya meneja, naye aliondoka miaka mingi iliyopita na hatukuwahi kupewa taarifa yoyote.

"Alichukuliwa Meneja Uendeshaji, Thomas Mushi, ambaye alishastaafu na ndiye aliyeandika barua ya kusudio la kuondoa waajiriwa wote. Yeye alishastaafu na mafao yake alishachukua, leo hii ndiye kaandika barua ya kusudio la kuondoa wafanyakazi wote," analalamika mmoja wa wafanyakazi wa kiwanda hicho.

Anabainisha kuwa tangu mwaka 2015, hakuna Meneja Mkuu na wanaona kamati maalum ikiitwa menejimenti ya juu ilhali ina watu wawili, akiwamo mwanasheria wa kampuni.

"Tunachotaka haki itendeke kwa wafanyakazi. Tumekuwa wazalendo kwa mali ya Watanzania. Tupewe stahiki zetu kwa haki," alisema mmoja wa wafanyakazi hao.

Mfanyakazi mwingine wa kiwanda hicho aliidokeza Nipashe kuwa nyumba za wafanyakazi kwa sasa zinapangishwa kwa kati ya Sh. 160,000 hadi 600,000 kwa mwezi, pia kuna nyumba za Urafiki zilizopangishwa kwa dola katika eneo la Masaki, Upanga, Kinondoni na Ilala. Zote za ghorofa.

"Tuna maswali mengi. Yanayofanyika serikali inayajua? Kama inajua kwanini inaacha hivi? Serikali imulike Urafiki. Ina mali nyingi. Nyumba za ghorofa za kisasa, maeneo ya wazi lakini hatujui fedha zinakwenda wapi. Lazima ichunguze fedha za Watanzania zisinufaishe wachache," anasisitiza mfanyakazi huyo.

### ACT-WAZALENDO

Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara wa ACT-Wazalendo, Halima Yusuf Nabalang'anya, akizungumzia suala hilo, anasema mkakati wa ujenzi wa viwanda nchini haueleweki.

"Wakati serikali inasema inaweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji kwa ajili ya kuhakikisha sekta ya viwanda inazalisha bidhaa zinazohitajika kwa wingi nchini ili kukidhi mahitaji na kuondoa utegemezi kutoka nje, mwenendo wa uwezo na uzalishaji wa viwanda vinavyojibu mahitaji ya watu wengi kama vile sukari, mafuta ya kula, nguo na mavazi, viwanda vya mbolea, saruji na sabuni haujibu wito huo.

"Viwanda vingi vya nguo, mafuta ya kula, sukari na hata saruji, vilibinafsishwa na baadaye vikageuzwa kuwa maghala ya kuhifadhi bidhaa kutoka nje. Viwanda kama Urafiki, Karibu Textile (KTM) vinaingia katika kundi hili. Kuna viwanda vya dawa za binadamu kama kile cha Keko, viwanda vya tumbaku na korosho.

"Kuuliwa kwa viwanda hivi kumeongeza utegemezi wa bidhaa muhimu kutoka nje kiasi cha kuondoa uhuru wetu wa kujiamulia juu ya mahitaji ya ndani. Tunategemea mbolea ya kuagiza kwa zaidi ya asilimia 95, nguo na mavazi kwa zaidi ya asilimia 90, sukari kwa asilimia zaidi ya 50, dawa asilimia 95 na bidhaa zingine," alisema.

Waziri Kivuli huyo anasema ni muhimu serikali kusimamia sekta ya viwanda kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya walio wengi, ifufue viwanda vya nguo, viatu na vifaa vya kilimo.

Baadhi ya wafanyabiashara waliozungumza na Nipashe, wanasema wanalazimika kuuza vitenge na kanga kutoka China kwa kuwa nchini hakuna viwanda vinavyozalisha kanga nzuri kama za Urafiki ambazo zilikuwa ni pamba kwa asilimia 100.

Kwa miaka mitatu sasa, Wizara ya Viwanda na Biashara inapowasilisha bungeni hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi, moja ya vipaumbele vyake ni kuendelea kufufua viwanda na kufanya mapitio ya mkakati wa pamba, nguo na mavazi pasi na kueleza ni vingapi vimefufuliwa.

Katibu wa Mtendaji wa Chama cha Wazalishaji wa Viwanda vya Nguo Tanzania (TECMAT), Adam Zuku, anasema chama hicho ni jukwaa linalowaleta pamoja kwenye sera na kutengeneza nguo kwa soko la ndani na nje. Walisajiliwa mwaka 2015 wakiwa na wanachama 20. Sasa wamebaki wanane. Urafiki si mwanachama wao.

Adam anasema Urafiki walikuwa wanatengeneza kanga, vitenge nguo za jeshi na sare za shule kwa nchi nzima. Wakati wa Vita vya Kagera, sare zote za jeshi zilitengenezwa Urafiki.

Anasema baada ya serikali kugundua kiwanda kinakufa, walitumwa kuchunguza ili kujua kiwanda kina hali gani kabla ya kumpa mwekezaji mpya na iliundwa timu, naye alichaguliwa kama mtaalamu.

"Wakati kikiwa chini ya mwekezaji wa Wachina sikupata nafasi ya kukitembelea, nilienda baadaye, nilipotembelea machozi yalinitoka. Sikuamini nilichokuwa ninakiona, niliona uharibifu mkubwa ambao siwezi kuuelezea.

"Mwaka 2012 tulivyokwenda kukagua, tulikuta mitambo yote ya AC (viyoyozi) imekufa, sababu kubwa ni kutumia maji ya chumvi kupoza mitambo. Nilichukulia ni kama hujuma kubwa kwa kiwanda.

"Sehemu iliyonisikitisha sana ni ya kuchanganya rangi, nilikuta inatumika caustic soda (magadi soda) ya kiwango cha chini ambayo tulikuta mabomba yameziba na walianza kubomoa sakafu ili kuzibua.

"Hii nilichukulia ni makusudi kuua kiwanda, ni sawa upeleke gari gereji ukute wameweka dizeli badala ya petroli halafu wanakwambia 'samahani'.

"Nilichoona Urafiki tangu wachina wafike, makadirio walikuwa wanashusha, mfano walipanga kuzalisha tani 32,000, mwaka unaofuata wanashusha badala ya kuweka makadirio ya juu, wamekaa miaka yote lakini uzalishaji ulikuwa unashuka na mwisho ukawa sifuri. Hii ninaona ilikuwa ni dalili nyingine ya hujuma," anaeleza.

### LUGHA ILIYOTUMIKA

Anabainisha kuwa mikataba ilikuwa imeandaliwa kwa lugha ya Kichina. Hata vikao vya bodi viliendeshwa kwa lugha hiyo, jambo ambalo lilipoteza maana na kutokea kutoelewana kwa kadri ya mtu alivyoelewa.

Adam anasema kanga za Urafiki zilisifika kwa ubora na zilidumu miaka mingi, lakini kinachoshuhudiwa sokoni leo ni kanga na vitenge kutoka China. Anazitaja ni ndogo. Haziyatoshi maumbo ya Waafrika.

"Kwa sasa vitenge, kanga ambavyo siyo pamba asilimia 100 vinatoka China, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lilitengeneza viwango vya kitaifa kwa kanga na vitenge vya Tanzania kwenye urefu, upana na uzito, lakini vinavyoingizwa nchini havina huo ubora," anasema.

Kwa mujibu wa katibu huyo, matatizo ya Urafiki yametengenezwa na wamefanikiwa kukiua na sasa Tanzania itakuwa soko la kanga na vitenge kutoka nje.

"Nguo ni kichocheo kikubwa cha mapinduzi ya viwanda duniani. Kila nchi iliyoendelea kwa viwanda ilipita katika mchakato wa viwanda na dunia watu wanavaa. Sisi tuna pamba, tunauza nje halafu tunanunua nguo. Tulikuwa na viwanda 33 na sasa vimebaki vinane," anaeleza.



Mbunge wa Same Mashariki, Anne Malecela akichangia hoja ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ya mwaka wa fedha wa 2023/2024, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jela miaka miwili kumtapeli mstaafu milioni 312/-

**Na Kulwa Mzee**

MFANYABIASHARA Perpetua Gondwe, amehukumiwa kifungo cha miaka miwili jela na baada ya kukiri kumtapeli mstaafu Sh. milioni 312 na kutakiwa kuzirejesha.

Pepetua alihukumiwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Ferdnand Kihwonde.

Kesi hiyo ilikuja jana na mshtakiwa aliomba kusomewa upya mashtaka ya kughushi na kujipatia kiasi hicho cha fedha kwa njia ya udanganyifu na hatimaye kukiri makosa.

Wakili wa Serikali, Grace Mwanga, alimsomea maelezo ya awali ambayo alikiri maelezo yote.

Mahakama ilitoa nafasi kwa pande zote mbili kuwasilisha hoja kabla haijatoa adhabu, ndipo upande wa Jamhuri ulipoomba apewe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia kama hizo.

"Mheshimiwa Hakimu ni rai yetu upande wa mashtaka, mshtakiwa apewe adhabu kali. Fedha alizochukua ni fedha za kustaafu alizokuwa kalipwa Ritha Remi na zingine alichukua kutoka kwa mume wake.

"Mheshimiwa mume baada ya kubaini walitapeliwa, suala hilo lilileta mgogoro na mume anaumwa mpaka sasa hivi,"alidai Mwanga.

Gondwe aliwasilisha ombi kwamba apunguziwe adhabu kwa madai kwamba ana mtoto mdogo alijifungua akiwa gerezani na ana watoto wengine watatu wanamtegemea pamoja na wazazi wake wako Kilombero.

Alidai anayo nia ya kurejesha fedha hizo akipata nafasi na kwamba kwa sasa anatakiwa kufanyiwa upasuaji wa mkono katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ilala ya Amana.

Mahakama baada ya kusikiliza hoja hizo, ilitoa adhabu kwa kosa la kwanza la kughushi kwamba mshtakiwa atatumikia kifungo cha miaka miwili na kosa la pili la kujipatia fedha pia atatumikia kifungo cha miaka miwili, adhabu hizo zinakwenda kwa pamoja.

Katika hati ya mashtaka, ilidaiwa Aprili 22, 2019 ndani ya mkoa na jiji la Dar es Salaam, kwa njia ya kudanganya, mshtakiwa alijipatia kiasi cha Sh. 312,429,000 kwa njia ya udanganyifu.

Alidaiwa kujipatia kiasi hicho cha fedha kutoka kwa Ritha Remi baada ya kudanganya kuwa fedha hizo zitatumika kwa ajili ya biashara wakati akijua si kweli.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa katika tarehe hiyo, mkoani Dar es Salaam, kwa lengo la kudanganya, alighushi namba ya utambulisho ya mlipakodi (TIN) ya Septemba 19, 2016 kwa lengo la kuonyesha kwamba ilitolewa na Kamishna wa Kodi za Ndani wa Mamlaka ya Mapato Tanzania wakati akijua si kweli.

# Ripoti tathmini uchumi vyombo vya habari kutolewa Novemba

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RIPOTI ya tathmini ya hali ya uchumi wa vyombo vya habari nchini inatarajiwa kutolewa Novemba, mwaka huu.

Wakati hayo yakisubiriwa, serikali ikiwataka waandishi wa habari na wadau wa tasnia hiyo kutoa ushirikiano kwa kamati husika ili kunusuru vyombo vya habari nchini.

Waziri wa Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Nape Nnauye, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi baada ya kukutana na Kamati ya Tathmini ya Hali ya Uchumi wa Vyombo vya Habari nchini.

"Nimekutaka na kamati hii awali tulikuwa tumeipa miezi mitatu lakini kutokana na umuhimu wa tasnia hii na maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, imeonekana kwamba jambo hili lisifanywe kwa kuharakishwa bali lifanywe kwa umakini wa hali ya juu ili kuleta mabadiliko katika tasnia hii," alisema Nape.

Waziri alisema kamati hiyo badala ya kuharakisha jambo hilo inapaswa kufanya utafiti wa kina kwa kuhusisha wadau wengi ili kupata maoni ambayo yatakuwa na manufaa na vyombo vya habari nchini.

"Jambo hili linasubiriwa sana na dunia. Watu wanataka kuona nini Tanzania inakwenda kufanya katika kuleta mageuzi kwenye tasnia hii ya vyombo vya habari nchini hivyo lazima tuje na kitu kinacholeta mabadiliko kwa vyombo vyetu vya habari nchini," alisema.

Aidha, alisema hadi sasa anaridhishwa na kazi ambayo inaendelea kufanywa na kamati hiyo kutokana na kushirikisha wataalamu kutoka nyanja mbalimbali ambao wameongeza tija katika tathmini hiyo.

"Kutokana na ramani ambayo kamati hii imeichora, hadi sasa inaonyesha ni kwa jinsi gani inakwenda kuleta mambo ambayo yatakwenda kujibu changamoto mbalimbali zinazoikabili tasnia hii ya habari.

"Hivyo basi nitowe wito kwa waandishi wa habari na wadau wengine wa habari nchini kutoa ushirikiano kwa kamati hii ili ifanikishe jambo hili na kuleta mabadiliko kwenye vyombo vya habari ambavyo vingi hivi sasa vipo hoi," alisema Nape.

Pia alisema wakati jambo hilo likiendele mchakato wa sheria ya vyombo vya habari pamoja na sera utaendelea na kama itaonekana kuna haja kufanyiwa maboresho yatafanywa.

Naye Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Tido Mhando, alisema yeye na wajumbe wote wamelivalia njuga suala hilo ili kusaidia vyombo vya habari na wanahabari nchini.

Pia alisema watahakikisha jambo hilo linakamilika ifikapo mwezi Novemba mwaka huu kwa mujibu wa muongozo waliopewa ili kulisaidia taifa.

"Matatizo ya vyombo vya habari yapo sehemu nyingi duniani inasikitisha sana kuona wanahabari nchini kuendelea kuwa ombaomba na kutegemea bahasha ili waishi na kutokuwa na uhakika wa kesho yao," alisisitiza Mhando.


HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VYOMBO VYA USAFIRI CHAKAVU**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kwa kushirikiana na Ofisi ya Msimamizi wa Mali za Serikali Mkoa wa Rukwa na Katavi wanawatangazia Wananchi wote kwamba watauza kwa njia ya Mnada wa hadhara likiwemo gari moja na pikipiki saba. Mnada utafanyika eneo la Bomani – Sumbawanga Mjini zilipokuwa Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga Mkabala na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga tarehe 30 Mei 2023 kuanzia saa 4:00 Asubuhi.

**Masharti ya mnada**

1. Chombo cha usafiri kitauzwa kama kilivyo na mahali kilipo
2. Atakayetaja bei ya juu kabla ya nyundo kugongwa ndiye atakayeuziwa Chombo chakavu cha usafiri
3. Aliyetaja bei ya juu sio lazima auziwe kama bei hiyo haijafika bei iliyotarajiwa
4. Mnunuzi atalazimika kulipa papohapo kiasi cha Asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya chombo cha usafiri alichonunua au Asilimia mia moja (100%). Aidha ndani ya siku kumi na nne (14) Mnunuzi anatakiwa awe amekamilisha malipo kwa Asilimia mia moja (100%) na akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi na 25% aliyolipa, na Chombo cha usafiri kitauzwa kwa Mnunuzi mwingine.
5. Mnunuzi yeyote atakaye taja bei ya juu na kushindwa kulipa kiasi husika atachukuliwa kuwa alikuwa na njama za kuharibu Mnada na hatua za Kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
6. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua kifaa alichonunua ndani ya masaa ishirini na nne (24) baada ya kukamilisha malipo.
7. Ruhusa ya kuangalia Vyombo vya usafiri Chakavu tajwa hapo juu itatolewa kwa muda wa siku moja ya tarehe 29 Mei 2023 kuanzia saa 02:00 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri.

**Herbert J. Mbise**
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**SUMBAWANGA.**
**22/05/2023**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni sawa Profesa Kabudi, ila tusikurupuke tutaumia

**DUNIA** inapoelekea ni wazi kuwa usafiri utakuwa ni wa injini za umeme na gesi. Ili kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya hali ya hewa, magari, treni, pikipiki za umeme ndiyo uelekeo sahihi.

Ni uhamasishaji unaofanywa na Mbunge wa Kilosa (CCM), Prof. Palamagamba Kabudi, wakati akichangia makadirio na mapato ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, bungeni jijini Dodoma, akisema Tanzania ijipange.

Wakati anaikumbusha wizara hiyo, Shirika la Kimataifa la Nishati (International Energy Agency), linasema idadi ya magari ya umeme kuanzia malori, mabasi na magari madogo kwenye barabara duniani imeongezeka kutoka milioni 11 hadi milioni 145 sasa.

Ongezeko hilo linachangiwa na maendeleo ya kiteknolojia katika mifumo ya usafirishaji pia sera zinazohamasisha kuachana na nishati za visikuku (fossils) kama mafuta na makaa ya mawe yanayochangia ongezeko la joto.

Kama anavyosema Prof. Kabudi, tunakubaliana naye kuwa Tanzania ni sehemu ya wimbi hili la usafiri wa umeme linalokua kwa kasi, ikumbukwe kwamba nchi za kiafrika tena majirani Kenya na Rwanda, zinatoa vivutio ikiwamo kupunguza kodi kuvutia uagizaji wa magari ya umeme na ujenzi wa viwanda vya kutengeneza magari, pikipiki na bajaji za umeme.

Katika miji yetu yote, mabasi makubwa kwa madogo, pikipiki na bajaji ndiyo njia kuu ya usafiri wa umma, ambayo bila shaka asilimia 90 ya uchafuzi wa hewa ya mijini inachangiwa na moshi wa injini hizo.

Katika miji mingi, mabasi hayo, bajaji na pikipiki hukadiriwa kuchangia asilimia 90 ya uchafuzi wa hewa.

Kwa hivyo, tunasema kumekucha juhudi za kuongeza matumizi ya magari ya umeme na gesi hazikwepeki na huko ndiko kuondoa 'carbon' au hewa ukaa na kuboresha hewa za miji na majiji yetu.

Hata hivyo, tutoe angalizo kuna mambo muhimu ya kushughulikia ili kupata tija kwenye usafiri wa magari ya umeme ambayo ndiyo yanayotazamwa duniani kote.

Tunaomba kuwakumbusha pia viongozi wetu wanaosimamia usafirishaji na mazingira kuamka, kwanza kudhibiti uingizaji holela wa magari kutoka ng'ambo yenye injini za mafuta, wamiliki wa Ulaya, Uarabuni na Marekani wanaponunua mapya ya umeme ili kuzuia Tanzania isiwe dampo.


Tunakumbusha kuwa ni muhimu kuwa makini kudhibiti magari ya mitumba ya umeme wanayoagizwa nchini kwa kuhakikisha kuwa inaingia mitumba yenye maisha marefu ya kutosha na iliyo bora.

Eneo jingine la muhimu ni uwezo wa kutupa kwa usalama betri za 'lithium-ion' zinazoendesha magari hayo. Tunashauri taifa lijipange mapema kwa vile zinahitajika kanuni isije kuwa kama betri za simu ambazo zimetapakaa kila kona na zinachafua mazingira.

Tunakumbusha kuwa Afrika ndilo soko kubwa zaidi la magari ya mitumba duniani na kwa mujibu wa Mpango wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa (UNEP), imegeuzwa dampo la magari mitumba, chakavu ya ubora duni.

Hata hivyo, UNEP inasema ni kama sikio la kufa, Afrika ikiwamo Tanzania haisikii dawa hadi leo ni Afrika Kusini, Misri na Sudan pekee zilizopiga marufuku uagizaji wa magari mitumba. Wakati nchi za magharibi zikijitahidi kuondoka kwenye injini za mafuta machafu na kutumia za umeme, magari yao mengi ya zamani yanatumwa Afrika, hivyo tuanze sasa kuchukua hatua za haraka kuepusha uchafuzi ambao ni tishio na hatari zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# 'Moto' Kariakoo uamshe ujio uongozi shirikishi

**UONGOZI** ni mfumo wa utawala ambao ulianza tangu enzi, hata maandiko matakatifu yanaeleza walikuwapo viongozi, lengo ni kuwa katika mstari mmoja, unaoelewana, kusikilizana na kupunguza kero.

Hembu fikiria mfumo huo, usingalikuwapo, kuanzia ngazi ya chini kwenye kitongoji, mtaa au kijiji, ujumbe na mawasiliano kwenye jamii ungefikaje? Hivyo kiongozi ni kiungo muhimu popote, iwe mwanasiasa, kiongozi wa mila, mhubiri wa Neno la Mungu, hata mkuu wa kaya.

Pamoja na hilo, uongozi shirikishi kwenye ngazi zote iwe kisiasa, kielimu na kijamii ndilo la muhimu, kwa kuwa wananchi ndiyo wanafahamu kinachowasibu mtaani, kijijini, sokoni hata katika usafiririshaji.

Wafanyabiashara wa sokoni Kariakoo jijini Dar es Salaam, hatua waliyoifikia na kuitisha mgomo inaonyesha pengo kwenye uongozi, iwapo awali viongozi wa ngazi zote hadi wizara wangekuwa karibu nao, ni wazi wasingechukua hatua hiyo.

Kuna cha kujifunza, mbali na kamati kuundwa kubaini sababu. Kuna darasa, kwanza kiongozi, ambaye anaiongoza jamii kwa kutumia muda wake mchache mara moja kwa mwezi au miezi mitatu, palipo na ufa atapabaini, akipatafutia suluhisho.

Taswira ya soko kuu hilo ni la kimataifa. Dosari ndogo husababisha hasara kiuchumi na wote kuathirika, kuanzia mlaji wa kwanza wa bidhaa zilizoko soko hilo hadi wa mwisho.

Mawasiliano kati ya kiongozi na anaowaongoza ni muhimu, ili kuweka mambo sawa, badala ya kusubiri kiongozi wa juu kitaifa kuitwa kufanya maamuzi.

Palipo na kundi kubwa pana mengi, na wanapitia changamoto lukuki. Kilichoonyeshwa na wafanyabiashara hao si tu kwenye sekta hiyo ya uchumi, kipo sekta zote, ila wanakosa pakusemea kutokana na utaratibu wa viongozi wali wengi, kudhani uongozi ni kukaa mbali na watawaliwa.

Unapokaa mbali na wananchi utayajuaje yaliyopo kisogoni! Kiongozi shirikishaji huwa karibu na anaowaongoza, akiwa na wajibu wa kuja na mbinu zinazopunguza au kuondoa matatizo.

Mfano mbunge, diwani, balozi, kiongozi wa mtaa ni wajibu wake kuwa karibu na wananchi, waliompa kura na si kusubiri kipindi cha kuutafuta uongozi.

Kwa vyovyote vile kiongozi aliyeegemea katika jamii anakubalika. Na utaratibu huo ukijengwa wananchi watajengeka na kufahamu mbivu na mbichi, wasiohongeka kwa rushwa ya aina yoyote.

Uwajibikaji kwenye nchi zinazoendelea ni duni, kuliko zilizoendelea na hii husababisha, uongozi kuonekana ni jambo analolimudu kila mmoja, hata ambaye si mtendaji.

Kilichoonyeshwa na Wanakariakoo, si jijini Dar es Salaam pekee, kinapatikana pia, nchi nzima na sekta zote. Viongozi wakae chonjo na kujenga mazoea ya kuwatembelea wanaowaongoza, ili kubaini wako kwenye mstari sahihi au la.

Katika jamii yapo masuala lukuki kuanzia usafi, ulipiaji huduma kadhaa ambao hauendi sawa, na kuwa kati ya changamoto zinazokwamisha na kuwa kero.

Mfano hivi karibuni, nilipoutumia usafiri wa mwendokasi kutoka kituo kikuu cha Gerezani hadi Kimara Mwisho, mamia ya abiria walijaa kwenye kituo hicho kikuu kwa takribani saa moja, hakuna taarifa yeyote, huku baadhi ya abiria wakishidwa kumudu kusimaa muda mrefu.

Baada ya muda abiria walianza mjadala kwa sauti ya chini, baadaye mazungumzo yalishika kasi tena kwa sauti ya juu. Mbaya zaidi ndani ya kituo hicho ni 'gereza' kwa sababu huna mbadala, inakupasa usubiri usafiri huo utake usitake kwa sababu umeshalipia nauli kati ya Shilingi 750 au zaidi.

Uongozi wa hapo ndipo walipoamua kutangaza kwamba uchache magari ndiyo unaosababaisha msongamano, hivyo wavute subira. Ndipo nilibaini mawasiliano na kupeana taarifa mapema ni muhimu kwa umma.

Viongozi wana cha kujifunza hatua zilizochukuliwa Kariakoo wawajibike wasiwe mamangi meza.

HABARI KITAIFA

## Wabunge waungana kudai kivuko bungeni

**Na Romana Mallya, DODOMA**

MBUNGE wa Kigoma Mjini, Kirumbe Ng'enda, amesema ameungana na wabunge wenzake akiwa mwenyekiti wao iwapo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi haitapeleka meli Ziwa Tanganyika, itakuwa mara ya mwisho kuunga mkono bajeti ya wizara hiyo.

Mbunge huyo aliyasema hayo juzi bungeni jijiji hapo, wakati akichangia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24.

"Leo Mheshimiwa Mwenyekiti ninataka nianze na meli katika Ziwa Tanganyika. Nimesikia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia meli ya Liemba ambayo sasa imesimama kwa miaka saba. Wananchi wa Ziwa Tanganyika wakiwa hawapati huduma kwamba itaanza kukarabatiwa mwezi Juni mwaka huu na kutachukua takribani miezi minane kukamilika na kurudi majini.

"Ninataka kumwambia Mheshimiwa waziri kwanza, hii kauli umeitoa hapa bungeni, sisi tunaiunga mkono. Na mimi niliyesimama hapa mbali ya kuwa ni Mbunge wa Kigoma Mjini.

Alisema kutokana na matatizo yaliyopo Ziwa Tanganyika ya huduma mbalimbali wametengeneza umoja wao wa wabunge wa mikoa ya Ziwa Tanganyika ambayo ni Kigoma, Rukwa na Katavi na yeye akiwa mwenyekiti wao.

"Nataka nikwambie hii ni mara ya mwisho kusimama katika Bunge kuunga mkono bajeti ya wizara yako kama hakutakuwa na meli kwenye Ziwa Tanganyika. Ninatumia maneno haya ili Watanzania wote wasikie, kama mpaka tutakapoingia kwenye bajeti nyingine meli hazitakuwapo Ziwa Tanganyika," alisema.

Alisema waliosimama kwenye umoja na kuishinikiza serikali Ziwa Victoria kwa sasa wana meli tano ambazo zinafanya kazi wakati Ziwa Tanganyika hakuna hata moja.

"Kwa namna yoyote na kwa shinikizo lolote hatutaunga mkono bajeti kama meli hazitakuwa ziwani mpaka tunakuja kwenye bajeti nyingine," alisema.

Pia alisema MV. Mwongozo imesimamishwa takribani miaka mitano kwa sababu ya MV Bukoba kuzama na sababu zikitajwa kuwa ni meli pacha.

"Kwa sababu ilipata ajali mkasimamisha na hii. Ni maneno ambayo ukimwambia mtu hawezi kuelewa. Kuna ndege ilipata ajali juzi hapa sijui mmesimamisha ndege zote za aina hiyo? Hii meli ilikuwa inafanya kazi na haikuwa na tatizo lolote na Ziwa Tanganyika kuna mawimbi makubwa kuliko Ziwa Victoria.

"Mmesimamisha mpaka leo hajapatikana mtu wa kuitengeneza hili ni jambo la aibu kwa wataalamu waliosomeshwa na taifa," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Ruvuma, Jackline Msongozi alisema; "Mheshimiwa Mwenyekiti daraja la Mitomoni, mwaka jana nilipiga magoti hapa. Mheshimiwa Mbawala (Mbarawa) wewe utapata laana na wana Ruvuma daraja lile halijajengwa watu wanaendelea kufa pale.

Kutokana na kukosea jina la Waziri, Mwenyekiti wa Bunge alimsahihisha na kumtaka akiendelea kuchangia asahihishe jina la Mbarawa na akiendelea na mchango wake mbunge huyo alisema, "Yeye anaelewa ndio maana anacheka, asante sana ninaunga mkono hoja."



Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Kiria Laizer (kulia), akiweka tofali kwenye ukuta katika ujenzi wa ofisi mpya za CCM Kata ya Orkesumet, alipotembelea na kamati ya siasa ya wilaya juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Samia ataka kuharakishwa uwekezaji elimu, afya Afrika

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka viongozi Afrika, watunga sera na wadau wengine wa maendeleo kuharakisha uwekezaji katika elimu, afya na ujuzi ili kulinda uzalishwaji wa nguvu kazi katika kanda hiyo ambayo ndiyo rasilimali yake kubwa.

Rais Samia ametoa wito huo mwishoni mwa wiki, katika hafla ya uzinduzi wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Rasilimali Watu Afrika (HCS), unaotarajiwa kufanyika Julai 25 na 26, mwaka huu, nchini.

Kaulimbiu ya mkutano huo ni 'Kuharakisha Ukuaji wa Uchumi wa Afrika: Kuongeza Tija kwa Vijana kwa Kuboresha Mafunzo na Ujuzi'.

Alisema wakati bara hilo likipambana na athari kubwa zilizotokana na janga la UVIKO-19, mfumuko wa bei na vipaumbele vya kifedha vinavyoshindana na bajeti finyu, wanaweza kutumiwa na ajenda zinazozingatia misaada ya haraka kutokana na migogoro hiyo na kupoteza mwelekeo wa uwekezaji muhimu wa rasilimali watu unaohitajika.

"Ninatoa wito kwa viongozi wenzangu wa kiafrika kutoondoa hatua hizi muhimu. Watu wetu ni muhimu katika kufungua matarajio yao na uwezo wa kiuchumi wa bara," alisema Rais Samia.

Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia wa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Victoria Kwakwa, alisema Mradi wa Mitaji ya Binadamu (HCP), ulizinduliwa na benki hiyo mwaka 2018 kama juhudi za kimataifa za kuharakisha uwekezaji bora kwa watu kwa usawa na ukuaji wa uchumi na nchi 87 barani humo zimejiunga.

Alisema mradi huo unatumia utetezi, kipimo na kazi ya uchambuzi ili kuongeza ufahamu na uhitaji wa afua za kujenga mtaji wa watu. Miongoni mwa uchanganuzi huo unajulikana kama Human Capital Index (HCI), ambao unabainisha mchango wa afya na elimu katika tija ya kizazi kijacho cha wafanyakazi.

Kwa mujibu wa Victoria, Afrika iliingia katika muongo uliopita ikiwa na upungufu mkubwa wa mtaji wa binadamu, ikilinganishwa na mabara mengine, wakati majanga ya hivi karibuni ikiwamo UVIKO-19 yakirudisha nyuma kujifunza, kuongeza pengo la ujuzi na changamoto za kiafya.


"Itawaleta pamoja viongozi kutoka barani kote ili kuzingatia umakini na kuteka ahadi zinazoonekana za kifedha na sera zinazoweka kipaumbele kuwekeza kwa watu kama kichocheo kikuu cha tija, uthabiti na ukuaji," alisema Victoria.

Alisema inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2050, Afrika itaongeza idadi ya watu wake mara mbili hadi bilioni 2.2, uwekezaji kwa wakati unaofaa katika elimu na afya ya wakazi wake unaweza kuchochea uzalishaji, ajira na kufungua uwezo mkubwa wa kiuchumi wa kikanda.

Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia wa Kanda ya Afrika Magharibi na Kati, Ousmane Diagana, alisema bara hilo linapaswa kuwekeza kwa wanawake, watoto, na vijana ili kuhakikisha usawa kwa kuwa ni moja ya misingi muhimu ya kufikia matokeo bora ya mtaji wa binadamu.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Vurugu wananchi, askari zaua mmoja na kujeruhi watu saba

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MTU mmoja amepoteza maisha na wengine saba kujeruhiwa vibaya kwenye vurugu zilizotokea jana katika Kijiji cha Jangwani, eneo la Mto wa Mbu, Monduli mkoani Arusha, baada ya kundi kubwa la wananchi kuandamana na kufanya uharibifu wa ofisi za serikali.

Waandamanaji hao wanadaiwa pia kuchana bendera ya taifa kutokana na kile kinachoelezwa ni kuchukizwa na madai ya kuzamishwa wavuvi wawili kwenye Ziwa Manyara na watu wanaohisiwa kuwa askari wa Hifadhi ya Taifa ya Manyara.

Jana Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi, (ACP) Justine Masejo, alithibitisha kuwa hadi sasa watu 12 wanashikiliwa na jeshi hilo wakihusishwa na vurugu hizo.

"Hilo tukio lilitokea Mei 22, mwaka huu, majira ya saa 5:40 asubuhi katika kitongoji cha Magomeni, kijiji cha Jangwani, eneo la Mto wa Mbu, wilayani Monduli. Wakati askari wa Hifadhi ya Taifa ya Manyara, wakiwa doria ya kawaida eneo la Ziwa Manyara, walikamata wavuvi watatu waliokuwa wakivua samaki katika maeneo yaliyozuiwa kwa uhifadhi.

"Sasa wakiwa doria, ghafla walijitokeza wavuvi wengine na kuzusha vurugu iliyosababisha askari hao wa uhifadhi kushindwa kuwachukua watuhumiwa hao na kwenda kutoa taarifa kituo cha polisi.

"Umati wa watu hao ulikwenda Ofisi ya Kijiji cha Jangwani na kufanya uharibifu mkubwa katika ofisi hiyo ya serikali kwa kuvunja madirisha na kuchana bendera ya taifa na kuondoka nayo. Hiyo yote, wanadai kuwa wavuvi wenzao wamezamishwa maji ziwani wakati wanakamatwa na askari wa uhifadhi," alisema.

Masejo alisema baada ya uharibifu huo, kundi hilo lilikwenda kwenye ofisi na makazi ya askari wa TANAPA (Shirika la Hifadhi za Taifa) yaliyoko Mto wa Mbu na kuharibu magari kwa kutumia marungu na mawe pamoja na kupanga mawe barabarani, kuzuia watumiaji wengine wa barabara wasiendelee na shughuli zao.

Kwa mujibu wa Kamanda Masejo, licha ya juhudi za kuwazuia kuingia ofisini na makazi hayo, watu hao waliendelea kupambana na askari wa uhifadhi na ndipo Jeshi la Polisi lilipoongeza nguvu, ili kuzuia madhara zaidi kwa binadamu na mali za watu binafsi na za serikali.

Kutokana na ghasia hizo, Kamanda Masejo, alisema mtu mmoja alifariki dunia na saba kujeruhiwa na kulazwa hospitalini (hakuitaja jina).

"Endapo watuhumiwa hawa watabainika kufanya vurugu hizo na ukweli kulingana na ushahidi watu hao walioutoa, watafikishwa mahakamani wakati wowote," alisisitiza.




Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli (wa pili kushoto), akikabidhi kifaa cha kazi kwa Amili Bago, baada ya kuhitimu mafunzo ya ufundi chini ya VETA mkoani Morogoro mwishoni mwa wiki. Wengine ni Meneja Mradi wa KCB 2jiajiri, Betty Muruve (wa tatu kushoto) na (kulia) Meneja Miradi wa 2jiajiri - Uendelezaji Ujuzi E4D Programu, Costantine Shirati. Kushoto ni Kaimu Katibu Tawala Wilaya ya Mvomero, Frazier Mang'ula. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Viwanda vya ndani kujengea uwezo

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amesema serikali itaendelea kuvijengea uwezo viwanda vya ndani vinavyozalisha saruji kabla bidhaa hiyo haijaruhusiwa kuwa kati ya bidhaa 10 zitakazoingia katika Soko Huru la Afrika (CFTA).

Aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam alipokutana na kufanya majadiliano na wazalishaji na wasambazaji wa saruji nchini katika kikao kilichojadili changamoto na fursa zilizopo katika sekta ya viwanda nchini.

"Dhamira yetu ni njema kuendelea kujenga uwezo ili tutakapoingia na bidhaa hii tuwe na uwezo mkubwa wa kupeleka katika eneo kubwa la Afrika," alisema waziri.

Aidha, Dk. Kijaji alisema katika kikao hicho wamejadili kwa kina changamoto ya upatikaji wa clinker ambayo ni malighafi muhimu inayotumika kutengeneza saruji, kuwa serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti kukabiliana nayo.

"Kumekuwa na malalamiko ya upatikanaji wa clinker ndani ya nchi yetu ambapo wapo wachache ambao wanaochukua malighafi hii kutoka nje ya nchi hivyo kwenye kikao hiki tumejadiliana na kukubaliana ni kipi kinachosababisha wazalishaji wetu kuagiza clinker nje ya nchi wakati viwanda vya ndani vina uwezo wa kuizalisha malighafi hiyo na kuuza nje ya nchi yetu," alisema.

Aliongeza kuwa uzalishaji wa bidhaa hiyo nchini utawapunguzia gharama wazalishaji na kutengeneza ajira ndani ya nchi.

Aliwahakikishia wazalishaji hao kuwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Bisashara kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati imeendelea kufanya kazi kuhakikisha viwanda vya ndani havikosi nishati ya umeme ambayo ni muhimu kwenye uzalishaji.

Tanzania ina viwanda vya saruji 14 vyenye uwezo wa kuzalisha saruji tani 10,000,000 na uwezo wa matumizi ya ndani ni tani 7,000,000.

Mkuu wa Mauzo na Masoko wa Kiwanda cha Saruji Dangote, Chux Mogbolu, aliishukuru serikali kwa kikao hicho muhimu ambacho kimejadili changamoto zinazoikabili sekta hiyo ikiwamo upatikanaji wa malighafi ya clinker.

Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda cha Saruji cha Nyati, Sajiv Kumar, aliishukuru wizara kupitia Waziri wake, Dk. Ashatu Kijaji kwa kuwasikiliza changamoto na maoni yao na kuahidi kufanyia kazi kwa ajili ya maendeleo ya sekta hiyo.

## Kampuni zamiminika Sabasaba

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) imesema kampuni 1,188 nchini na 112 za nje ya nchi zimethibitisha kushiriki Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, yanayotarajiwa kuanza Juni 28 hadi Julai 13, mwaka huu.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Biashara wa TanTrade, Fortunatus Mhambe, alisema hadi sasa nchi 14, ikiwamo China na Umoja wa Falme za Kiarabu zimethibitisha kushiriki katika maonesho hayo yenye kaulimbiu "Tanzania, mahali sahihi pa biashara na uwekezaji."

Alisema lengo kuu la maonyesho hayo ni kuwakutanisha wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi na kuwapa fursa ya kutangaza bidhaa na huduma zao pamoja na kutafuta masoko mbalimbali.

Alisema maonyesho ya mwaka huu yanatarajiwa kuboreshwa zaidi ikiwamo kuweka maeneo ya kuvutia na kujifunza zaidi kwa washiriki na watembeleaji wake maeneo maalumu kama Sabasaba Expo Village, lengo likiwa ni kutangaza fursa zilizopo katika sekta mbalimbali.


Mkurugenzi wa kampuni inayozalisha bidhaa zitokanazo na karanga, Agatha Laizer, alisema maonyesho hayo ya Sabasaba ni sehemu ya wafanyabiashara kupiga hatua kwa kutumia majukwaa tofauti.

## Apotea wakati akienda kuswali msikitini

**Na Mwandishi Wetu**

AMADI Juma mwenye miaka 25 (pichani) mkazi wa Bomba Mbili, Kata ya Mpijimagohe jijini Dar es Salaam, amepotea Aprili 28, mwaka huu wakati anakwenda kuswali swala ya mchana katika Msikiti wa Mwanzo Mgumu ulipo eneo hilo.

Mama wa kijana huyo, Zuhura Omari, alisema Amadi aliondoka nyumbani saa sita kamili mchana na kuelekea msikitini, lakini hakurudi tena tofauti na siku zingine.



Aidha, alisema kijana huyo ana tatizo la akili na wanahisi kuwa alikwenda kuswali kwenye msikiti mwingine na kushindwa kurejea nyumbani kwa kuwa alikuwa akifanya hivyo siku za nyuma na anapopotea hurudishwa na wasamaria wema wanaomfahamu.

Alisema baada ya kumtafuta kwa siku mbili bila mafanikio walikwenda kutoa taarifa kwenye Kituo cha Polisi cha Kivule na kupewa namba ya RB, KIV/ RB/455/2023 na kuomba yeyote atakayemuona kutoa taarifa polisi au kupiga namba 0621060466.





# Dawa za asili chanzo ongezeko wagonjwa shinikizo la damu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WATAALAMU wa tiba na uchunguzi wa afya, wamefichua siri ya ongezeko la wagonjwa wa shinikizo la juu la damu katika Mkoa wa Manyara kwamba linachochewa na wagonjwa kuamini zaidi dawa za asili.

Kaimu mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya mkoa huo, Dk. Yesige Mutajwaa, alisema ugonjwa huo ndiyo sababu kubwa ya vihatarishi vya ugonjwa wa kiharusi, shambulio la moyo, moyo kushindwa kufanya kazi na kutuna kwa ukuta wa mishipa ya damu.

Dk. Mutajwaa alieleza hayo jana wakati jopo la madaktari bingwa wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), ilipokutana na watumishi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara na wananchi waliofika kufanya uchunguzi wa ugonjwa huo.

"Wagonjwa wengi tunaowagundua baada ya kuwapima, wengi wanakuwa hawajisikii dalili za kuumwa; hivyo tukiwaambia wana shinikizo la juu la damu hawakubali na wanaacha kuchukua dawa zilizothibitishwa kisayansi na wanahamia kwenye matumizi ya dawa za asili au miti shamba kama wanavyoita wenyewe," alisema.

Kiongozi wa jopo la madaktari hao, Daktari Bingwa na Mkuu wa Idara ya Utafiti na Mafunzo wa JKCI, Dk. Pedro Pallangyo, akizungumzia kampeni hiyo waliyoianzisha, alisema wamepanga kuvifikia vituo vya afya 600 nchini pamoja na watumishi wa kada hiyo 2,000 ili kuwanoa na kuwapa mbinu za kukabiliana na ongezeko la wagonjwa hao.

"Ili kudhibiti ugonjwa huo, JKCI tumeshafika katika mikoa 10 nchini hadi sasa kwa ajili ya kutoa elimu kwa watumishi wa kada ya afya, juu ya namna ya kutibu ugonjwa huo," alisema Dk. Pallangyo.

Aidha, Mratibu wa Magonjwa Yasiyoambukiza wa Wizara ya Afya, Dk. Anzibert Rugakingira, alisema takwimu zinaonyesha kuwa wagonjwa shinikizo la juu la damu wanaongezeka, ambapo mwaka 2017 walikuwa na wagonjwa milioni 2.535 na hadi kufikia mwaka 2021 waliongezeka na kufikia wagonjwa milioni 3.4.

Katika kikao kazi hicho, Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Dk. Mugisha Nkoronko, alisema ni vizuri Watanzania wakazingatia ushauri wa kitaalamu na kuepuka matumizi ya chumvi nyingi, sukari na pombe ili kuukwepa ugonjwa huo.

# Shughuli za kibinadamu zaharibu chemchemi ya Kibola

**Na Godfrey Mushi,** ARUMERU

SHUGHULI za kibinadamu zinazoendelea kuchipua kwa kasi katika chemchemi ya maji ya Kibola iliyoko Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, zinatishia kutoweka kwa chanzo hicho kinachotegemewa na zaidi ya wananchi 26,737.

**Chemchemi hiyo inawanufaisha wananchi wa vijiji vya Sangananu na Nkoanekoli katika Tarafa ya Poli wilayani humo.**

Chemchemi hiyo inawanufaisha wananchi wa vijiji vya Sangananu na Nkoanekoli katika Tarafa ya Poli wilayani humo.

Akizungumzia kampeni hiyo jana, Mkurugenzi wa Bodi ya Maji ya Bonde la Pangani, Segule Segule, alisema wameamua kuzuia shughuli za binadamu katika eneo hilo na kupanda miti rafiki ili kukihifadhi chanzo hicho.

"Shughuli za kibinadamu ni pamoja na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni, mkaa au mahitaji ya ujenzi, mifugo, uchimbaji mchanga, ujenzi usiozingatia taratibu za mipango miji na kilimo kisicho endelevu," alisema.

Baada ya kampeni hiyo, Diwani wa Nkoanekoli, Shari Pallangyo, alisema shughuli za binadamu zinachangia mabadiliko ya tabianchi, ambalo husababisha kubadilika kwa mfumo mzima wa hali ya hewa.

Kampeni hiyo ilihusisha ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Kata ya Nkoanekoli, Jumuiya ya Watumia Maji ya Kikuletwa ya Juu, watendaji na wananchi wa vijiji vya Sangananu na Nkoanekoli.

Segule alisema Bodi ya Maji Bonde la Pangani inaendelea na jitihada za kulihifadhi korongo la Mto Nduruma lililodabuliwa baada ya kupoteza mkondo wake.

"Katika eneo hilo, Bodi ya Maji Bonde la Pangani, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ikiwamo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, imefanikiwa kuotesha miti 1,000 katika kingo za Mto Nduruma, kama sehemu ya kuendeleza jitihada za ulinzi wa chanzo hicho muhimu cha maji katika kidakio cha Kikuletwa," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Emmanuela Kaganda, amewaonya wanaoendesha shughuli za binadamu katika maeneo hayo, akisisitiza shughuli za kibinadamu kuepukwa, kwa kuwa zimekuwa zikisababisha mafuriko katika kata za Shambarai Burka na Mbuguni.



Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Kisare Makori, akipanda mti wa mfano huku akisaidiwa na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mary Goreti, Sista Clementina Kachweka (kushoto), baada ya kupokea miche ya miti 2,000 kutoka kwa shule hiyo jana, kama sehemu ya kampeni ya upandaji miti. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Majangili sasa kusakwa kwa mfumo wa kidijitali

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATUHUMIWA wa ujangili katika eneo la ikolojia ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Manyara, wataanza kusakwa kwa kutumia mfumo maalumu wa kidijitali, maarufu SMART.

Mfumo huo hutumika kukusanya taarifa, picha, kuzihifadhi na kuzituma kwenye kanzidata kwa usahihi.

Jana, ofisa data, usomaji ramani na ripoti za kidigitali wa Taasisi ya Friedkin Conservation Fund, Macarios Gisberth, alisema mfumo huo utarahisisha kuwadhibiti majangili kabla ya kuua wanyamapori ambao ni rasilimali za taifa.

Alikuwa akizungumza na askari wa wanyamapori wa Burunge-WMA, askari wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati na askari wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Nchini (TAWA) kuhusu matumizi ya mfumo huo.

"Mfumo huo wa kisasa utaanza kutumika mwaka huu katika eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Burunge, inayotekeleza Mradi wa Uhifadhi Maliasili, kwa udhamini wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID).

"Kimsingi, mfumo huu unatumia programu maalum, ambayo imewekwa katika simu za mkononi na kompyuta na una uwezo wa kupiga picha, kutunza kumbukumbu ya eneo la tukio na kuzituma kwa uharaka.

Zaidi aliongeza: "Huu mfumo pia, utawezesha kufanyika doria katika hifadhi za wanyamapori na kupata taarifa za matukio ya ujangili kabla haujatendeka, matukio ya uvamizi wa mifugo na uharibifu wa mazingira."

Vilevile, Ofisa Mradi wa Tuhifadhi Mazingira, unaotekelezwa na Taasisi ya Chemchem eneo la Burunge-WMA, Martin Mng'on'go, alisema katika mradi huo, askari wanaofanya katika eneo hilo watakuwa wakitumia mfumo huo kukabiliana na ujangili.

"Tayari askari wamejengewa uwezo wa kufanya doria kwa kutumia mfumo wa SMART, kuwachunguza majangili na kuwakamata kirahisi zaidi," alisema.

Ofisa Doria wa TAWA, Gabriel Charles, alisema mfumo huo wa kisasa ni suluhu jinsi ya kukabiliana na majangili.

Gabriel alisema: "Mfumo huu tumeona jinsi utakavyorahisisha upangaji mzuri wa doria, kukusanya taarifa za uhalifu na kuzifanyia kazi."

Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Babati, Godluck Kalambani, alisema mfumo huo utasaidia uchakataji wa taarifa na utoaji taarifa sahihi ikiwapo eneo ambalo mtuhumiwa ataonekana na hivyo kukamatwa kabla ya kutenda uhalifu.



# Pamba kupimwa kidijitali kudhibiti wizi katika vipimo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WIZARA ya Kilimo imetambulisha mfumo mpya wa mizani ya kidigitali ambao itaunganishwa na mizani ya kupima pamba ikiwa ni njia sahihi itakayoongeza tija katika ununuzi wa zao hilo na kudhibiti vitendo vya wizi.

Mizani inatarajiwa kuanza kutumika katika msimu huu ambako itasaidia kuwasajili wakulima wote katika mfumo huo maalumu na kila mkulima atakuwa na uwezo wa kutambua kiasi gani cha pamba ameuza katika masoko yatayofanyika katika vituo ambavyo vitatangazwa na Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU).

Katika mfumo huo kila mkulima atachukuliwa alama za vidole, ramani za mashamba yao, ukubwa wa shamba pamoja na aina ya mazao anayolima katika eneo hilo, ili kuwapatia fursa wakulima kutangaza mazao mengine wanayolima ukiachilia mbali na zao hilo na kujipatia kipato cha kaya.

**Kilo zitakazosoma kwenye mizani ndizo zitakasoma katika mfumo huo, hivyo hakuna mkulima yeyote atakayeibiwa hata nusu kilo ya pamba wakati wa mauzo.**

Akitoa mafunzo juu ya matumizi ya mfumo huo mpya juzi, Meneja wa Biashara kutoka Kampuni ya Mkulima Hub, Fakili Shaibu, kwa baadhi ya wakulima na viongozi wa vyama vya msingi na viongozi wa zao hilo wilayani Kahama mkoani Shinyanga alisema, mafunzo hayo wanayatoa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kwa lengo la kumsaidia mkulima asiendelee kuibiwa.

Alisema, usajili na uchukuaji wa taarifa za mkulima wa zao hilo utatumika mfumo wa usimamizi wa vyama vya ushirika nchini, kabla ya mauzo atangaliwa majina yake kama amesajiliwa ndipo atapima pamba yake.

Alisema kilo zitakazosoma kwenye mizani ndizo zitakasoma katika mfumo huo, hivyo hakuna mkulima yeyote atakayeibiwa hata nusu kilo ya pamba wakati wa mauzo.

Mrajisi Msaidizi wa Mkoa wa Shinyanga, Hilda Boniphace, alisema wanunuzi watakuwa wanawaona wakulima wote katika mfumo huo na kiasi cha pamba kilichopatikana katika msimu na kuondokana na wanunuzi waliozoeleka.

Colletha Mashimba ni mkulima kutoka wilayani Kahama alisema wanapokuwa sokoni katika mauzo hata ikipatikana nusu kilo walikuwa wakiandikiwa malipo na kwa mfumo huo wanatarajia kulipwa hadi pointi zitakazopatikana ambazo walikuwa hawaandikiwi malipo yake.



Meneja Mkuu wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Cheick Sangare (kushoto), akikabidhi zawadi ya koti la kinga ya ajali kwa mmoja wa waendesha punda wa kubeba mizigo wakati wa mafunzo ya uhamasishaji usalama kwa jamii yaliyoandaliwa na kampuni hiyo katika viwanja vya Shule ya Msingi Kakola, wilayani Msalala, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yabaini madudu ujenzi madarasa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JUMUIYA ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga Mjini, imebaini ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Msingi Msufini iliyopo Kata ya Ndala Manispaa ya Shinyanga kujengwa chini ya kiwango.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Fue Mrindoko, alisema katika ziara yao juzi ya kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, walibaini ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika shule hiyo yamejengwa chini ya kiwango, hali ambayo ni hatari kwa usalama wa wanafunzi.

Alisema walichokibaini katika ujenzi huo ni kwamba tofali zake siyo imara, kutokana na kupukutika kama biskuti, hayana saruji ya kutosha, kitendo ambacho kina ashiria kuna ufujaji wa fedha.

"Tunaomba wahusika wa ujenzi huu wa vyumba vya madarasa katika shule hii walifanyie kazi suala maana ni hatari kwa usalama wa wanafunzi watakuja kuangukiwa na majengo hayo," alisema Mrindoko.

Naye Katibu wa Jumuiya hiyo Wilaya ya Shinyanga Mjini, Doris Kibabi, alisema CCM haikubaliani na ujenzi huo wa madarasa kuendelea bali usimame kwanza hadi pale mapungufu hayo yatakaporekebishwa kwa lengo la kuchukua tahadhari mapema na kulinda usalama wa wanafunzi.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Msufini, Godfrey Jebele, alikiri kuwepo na mapungufu katika ujenzi wa vyumba hivyo vitatu vya madarasa akisema matofali yake ni kweli yanapukutika.

Hivyo aliahidi kulifanyika kazi, huku akibainisha gharama za ujenzi wake kuwa ni Sh. milioni 84.6 na ulianza Mei 15, mwaka huu kupitia mradi wa boost.

# TAKUKURU yapokea malalamiko 120, h/shauri zaongoza

**Na Titus Mwombeki,** KAGERA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera imesema imepokea taarifa za malalamiko ya vitendo vya rushwa 120 kutoka katika sekta mbalimbali mkoani humo.

Imesema halmashauri zimeongoza kwa kuwa na malalamiko 48 ikifuatiwa idara ya afya 10, elimu tisa, TANESCO nane na polisi matano huku kati ya malalamiko hayo baadhi yamefanyiwa kazi na mengine yapo katika hatua mbalimbali.

Taarifa hiyo ilitolewa juzi na Kaimu Mkuu wa TAKUKURU mkoani humo, Ezekia Sinkala wakati akitoa taarifa juu ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo kwa kipindi cha miezi mitatu.

Alieleza kuwa taasisi hiyo inaendelea kufanyia kazi taarifa zote zinazopokelewa ili kuhakikisha wanadhibiti vitendo vya rushwa katika taasisi za umma.

Katika hatua nyingine Sinkala alisema TAKUKURU baada ya kufanya uchunguzi walibaini mapungufu katika miradi sita ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 1.5 kati ya miradi 52 yenye thamani ya zaidi Sh. bilioni tisa.

"Miradi iliyobainika kuwa na mapungufu ni mradi wa barabara ya Nyakahanga -Nyabiyonza ulibainika kutokuwa mifereji ya kupitisha maji, ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje Zahanati ya Buganguzi ulibainika kuwa na mapungufu kwenye gypsum, vifaa vinavyonunuliwa haviingizwi stoo pamoja na ujenzi wa madarasa katika shule za sekondari na miradi ya maji tulibaini kuwa masharti ya mikataba hayazingatiwi," alisema.

Sambamba na hilo alisema katika kipindi cha Aprili mpaka Juni mwaka huu TAKUKURU mkoani humo wamejiwekea malengo ya kutekeleza vipaumbele ikiwa ni pamoja na kuendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuziba mianya ya ufujaji wa fedha za umma.

Pia alisema imejipanga kuelimisha umma kwa kutumia njia mbalimbali pamoja na kutatua kero kwenye jamii kupitia programu ya TAKUKURU RAFIKI.

**Katika kipindi cha Aprili mpaka Juni mwaka huu TAKUKURU mkoani humo wamejiwekea malengo ya kutekeleza vipaumbele ikiwa ni pamoja na kuendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuziba mianya ya ufujaji wa fedha za umma.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

## HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI MHE. PROF MAKAME MNYAA MBARAWA (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24




MHE. PROF. MAKAME M. MBARAWA (MB)
WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI

MHE. ENG. GODFREY M. KASEKENYA (MB)
NAIBU WAZIRI WA UJENZI

MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE (MB)
NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI

BALOZI ENG. AISHA S. AMOUR
KATIBU MKUU SEKTA YA UJENZI

BW. GABRIEL J. MIGIRE
KATIBU MKUU SEKTA YA UCHUKUZI

BW. LUDOVICK J. NDUHIYE
NAIBU KATIBU MKUU SEKTA YA UJENZI

DKT. ALLY S. POSSI
NAIBU KATIBU MKUU SEKTA YA UCHUKUZI

JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI, MHESHIMIWA PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

**A. UTANGULIZI**

1. Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/24.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo.

3. Mheshimiwa Spika, naomba kuungana na Bunge lako Tukufu katika kumpongeza kwa dhati Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka miwili katika kutuongoza kwa umahiri na mafanikio makubwa.

4. Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Makamu wa Rais kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika kuongoza nchi yetu.

5. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na makini.

6. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kazi kubwa unayoifanya ya kusimamia na kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi mkubwa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb), Naibu Spika kwa kuendelea kutekeleza vyema shughuli za Bunge. Vilevile, nichukue fursa hii kuwapongeza Wenyeviti Wote wa Bunge kwa kuchaguliwa kwao. Tunawaahidi ushirikiano katika kutimiza wajibu wa kusimamia na kuliongoza Bunge letu.

7. Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini katika kutekeleza majukumu yangu nikiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi tangu aliponiteua tarehe 12 Septemba, 2021. Ninaomba kumhakikishia kuwa, nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uwezo na uaminifu mkubwa ili kuliletea Taifa letu maendeleo. Ninamuahidi kuwa nitatumia weledi, maarifa na uwezo wangu wote katika kutekeleza wajibu wangu kwa ufanisi mkubwa.

8. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini kwa kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Aidha, nawapongeza Wajumbe wote walioteuliwa kwenye Kamati hii. Nichukue fursa hii kuishukuru Kamati hii kwa kuendelea kutoa ushauri na kuisimamia Wizara.

9. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kutoa salamu za pole kwa Bunge lako Tukufu na wote walioguswa na kifo cha Mbunge mwenzetu Mhe. Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Zanzibar. Tutaendelea kuthamini na kuuenzi mchango wake katika Bunge hili na Taifa kwa ujumla. Aidha, nimpongeze Mhe. Abdul Yussuf Maalim kwa kuaminiwa na wananchi kuwa Mbunge wa Jimbo la Amani.

10. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/23 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2023/24.

**B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

11. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imegawanywa katika mafungu mawili kibajeti ambayo ni Fungu 98 (Sekta ya Ujenzi) na Fungu 62 (Sekta ya Uchukuzi). Nitaanza na maelezo kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa Sekta ya Ujenzi ikifuatiwa na Sekta ya Uchukuzi.

**B-1: SEKTA YA UJENZI**

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

12. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/23, Sekta ya Ujenzi ilitengewa jumla ya Shilingi Bilion 44.293 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi Aprili, 2023 jumla ya Shilingi Bilion 32.893, sawa na asilimia 74.26 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

13. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo, katika mwaka wa fedha 2022/23, Sekta ya Ujenzi ilitengewa Shilingi Trilioni 1.377. Kiasi hicho kinajumuisha Shilingi Trilioni 1.124 fedha za ndani na Shilingi Bilioni 252.965 fedha za nje. Fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Funds) ni Shilingi Bilioni 777.785 na kutoka Mfuko wa Barabara ni Shilingi Bilioni 599.756.

Hadi Aprili, 2023 fedha zilizopokelewa ni Shilingi Trilioni 1.312 sawa na asilimia 95.3 ya fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/23. Kati ya fedha hizi, Shilingi Trilioni 1.069 ni fedha za ndani na Shilingi Bilioni 243.321 ni fedha za nje.

14. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuipongeza na kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kulipa hati za madai ya Makandarasi na Washauri Elekezi kwa wakati.

Aidha, kutokana na malipo hayo kufanyika kwa wakati, kasi ya utekelezaji wa miradi imeongezeka. Vilevile tunaishukuru sana Serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuwalipa Makandarasi na Washauri Elekezi ambapo katika mwaka wa fedha 2022/23 jumla ya Shilingi 184.459 zimetolewa kwa ajili ya malipo ya madeni.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Miradi ya Barabara na Madaraja**

15. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/23, miradi ya barabara kuu iliyopangwa kutekelezwa ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 470 pamoja na ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 33.

Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa madaraja makubwa manne (4): Daraja la Kigongo – Busisi, Mwanza; Daraja la Gerezani (Dar es Salaam), Daraja la Pangani (Tanga) na Daraja la Wami (Pwani).

16. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2023, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 179.18 umekamilika na ujenzi wa kilometa 290.82 unaendelea. Aidha, ujenzi wa madaraja makubwa mawili (2) ya Wami na Gerezani umekamilika. Vilevile, ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi, Mwanza umefikia asilimia 72 na ujenzi wa daraja la Pangani (Tanga) umefikia asilimia 3.

17. Mheshimiwa Spika, miradi ya barabara za mikoa iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/23 ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 103.01. Kazi nyingine ni kufanya ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara zenye urefu wa kilometa 1,042.43.

18. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2023 jumla ya kilometa 23.11 za barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometa 253.67 zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe.

**Miradi ya Barabara na Madaraja Iliyokamilika**

19. Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweza kupiga hatua kubwa ya mafanikio katika eneo la ujenzi wa barabara na madaraja.

Katika kipindi chake cha miaka miwili wa uongozi wa Mheshimiwa Rais, barabara katika maeneo mbalimbali zimejengwa na kukamilika. Barabara hizo ni pamoja na:-

i). Barabara ya Loliondo – Mto wa Mbu (km 201); Sehemu ya Waso – Sale Jct (km 49) mkoani Arusha;
ii). Barabara ya Morocco – Mwenge (km 4.3) kutoka Njia tano hadi Sita (km 3.2) Mkoani Dar es Salaam;
iii). Barabara ya Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98); Sehemu ya Mbande – Kongwa Jct (km 5.80) Mkoani Dodoma;
iv). Barabara ya Tabora – Koga – Mpanda; Sehemu ya 3: Kasinde – Mpanda (km 108) pamoja na kipande cha Barabara ya Urwira (km 3.7) Mkoani Katavi;
v). Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 268); Sehemu za Kidahwe – Kasulu (km 63) na Kakonko – Nyakanazi (km 50) Mkoani Kigoma;
vi). Barabara ya Bulamba – Kisorya (km 51) Mkoani Mara;
vii). Barabara ya Makutano – Nyamuswa – Ikoma Gate (km 153); Sehemu ya Makutano – Sanzate (km 50) Mkoani Mara;
viii). Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela; Sehemu ya Kuseni – Suguta (km 5) Mkoani Mara;
ix). Barabara ya Chunya – Makongorosi (km 39) Mkoani Mbeya;
x). Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi (km 210); Sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) Mkoani Mtwara;
xi). Barabara ya Njombe – Ndulamo – Makete (km 107.4) Mkoani Njombe;
xii). Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda; Sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) Mkoani Njombe;
xiii). Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112) Mkoani Rukwa;
xiv). Barabara ya Masasi – Songea Mbamba Bay; Sehemu ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66) Mkoani Ruvuma;
xv). Barabara ya Mpemba – Isongole (km 50.3) Mkoani Songwe;
xvi). Barabara ya Urambo – Kaliua – Ilunde – Uvinza; Sehemu ya Urambo – Kaliua (km 28) Mkoani Tabora;
xvii). Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora; Sehemu ya Nyahua – Chaya (km 85) Mkoani Tabora; na
xviii). Barabara ya Tabora – Koga – Mpanda; Sehemu Usesula – Komanga (km 108) pamoja na Sehemu ya Komanga – Kasinde (km 108) pamoja na Inyonga Spur (km 4.8).

20. Mheshimiwa Spika, Aidha, kuna miradi mbalimbali mikubwa ya ujenzi wa barabara inayoendelea na iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa:

i). Barabara ya Mianzini – Olemringaringa – Ngaramtoni Juu na Olemringaringa – Sambasha/Timbolo (km 18) – Kazi za ujenzi zinaendelea na zimefikia asilimia 18 Mkoani Arusha;
ii). Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha kuwa Njia Nane (8 lanes), (km 19.2) na Madaraja matatu ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji Mkoani Dar es Salaam;
iii). Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka; Awamu ya Pili (BRT Phase II) (km 19.3) na Awamu ya Tatu (Phase III): Nyerere Road corridor kutoka CBD - Gongolamboto (km 23.33) Mkoani Dar es Salaam;
iv). Barabara za Mzunguko wa Nje Jijini Dodoma (Dodoma City Outer Ring Roads); Sehemu ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.30) (Lot 1) na Sehemu ya Ihumwa – Dry Port – Matumbulu – Nala (Km 60.00) (Lot 2) Mkoani Dodoma;
v). Barabara ya Kumunazi – Bugene – Kasulo na Kyaka – Mutukula (km 124); Sehemu ya Bugene – Burigi Chato National Park (km 60); Mkoani Kagera;
vi). Barabara ya Kabingo – Kasulu – Manyovu (km 260.0); sehemu za Kanyani Junction – Mvugwe (km 70.5); Mvugwe – Nduta Junction (km 59.35); Kibondo Junction – Kabingo (km 62.5); Nduta Junction – Kibondo (km 25.9) na Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini (km 68) mkoani Kigoma;
vii). Barabara ya Kazilambwa – Chagu (km 36) mkoani Kigoma;
viii). Barabara ya Malagarasi – Ilunde – Uvinza (km 51.1); Mkoani Kigoma;
ix). Barabara ya Dumila – Kilosa; Sehemu ya

Ludewa – Kilosa (km 18) mkoani Morogoro;

x). Barabara ya Mikumi – Kidatu – Ifakara; Sehemu ya Kidatu – Ifakara (km 66.9): Mkoani Morogoro;

xi). Barabara ya Karatu – Mbulu – Hydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389); Sehemu ya Mbulu – Garbabi (km 25) Mkoani Manyara;

xii). Barabara ya Tarime – Mugumu (km 87.14); Sehemu ya Tarime – Nyamwaga (Lot 1: Mogabiri - Nyamongo) (km 25) Mkoani Mara;

xiii). Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 56.4) Mkoani Mara;

xiv). Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda, Mkoani Njombe;

xv). Barabara ya Tanga – Pangani – Mkange; Sehemu ya Tanga – Pangani (km 50) na Sehemu ya Tungamaa – Mkange (km 95.2) Mkoani Tanga; na

xvi). Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kwamtoro – Singida (km 434.33) Sehemu ya Handeni – Mafuleta (km 20): Ujenzi unaendelea na umefikia asilimia 11; Sehemu ya Mafuleta – Kileguru (km 30): Taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi zinaendelea.

21. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi wa madaraja jumla ya madaraja makubwa nane (8) yamejengwa na kukamilika ambayo ni:

i). Daraja la Wami (Pwani),
ii). Daraja la Tanzanite (DSM),
iii). Daraja la Gerezani (DSM),
iv). Daraja la Mpwapwa (Dodoma),
v). Daraja la Kiegeya (Morogoro),
vi). Daraja la Ruhuhu (Ruvuma),
vii). Daraja la Kitengule (Kagera) na
viii). Daraja la Msingi (Singida).

**Miradi ya Barabara, Madaraja na Viwanja vya Ndege Iliyosainiwa Mwaka wa Fedha 2022/23**

22. Mheshimiwa Spika, mikataba ya ujenzi na ukarabati wa miradi mbalimbali ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege ilisainiwa katika mwaka wa fedha 2022/23. Miradi hiyo ni ujenzi wa barabara za Lusahunga – Rusumo (km 92); Kitulo – Iniho (km 36.3); Sengerema – Nyehunge (km 54); Utete – Nyamwage (km 33.7); Kibondo – Mabamba (km 48); Igawa – Songwe – Tunduma Sehemu ya Uyole – Ifisi - Airport (km 32); Ibanda – Itungi Port (km 26); Kajunjumele – Kiwira Port (km 6); Barabara unganishi katika daraja la Sibiti (km 24.83) na barabara ya Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa sehemu ya Noranga – Doroto (km 6) na Itigi – Mkiwa (km 25.569). Miradi mingine ni ujenzi wa Madaraja ya Mpiji Chini na Mbambe. Aidha, mikataba ya miradi ya ujenzi wa Viwanja vya Ndege iliyosainiwa ni ya viwanja vya ndege vya Kigoma na Sumbawanga. Utekelezaji wa miradi hii uko katika hatua za maandalizi ya kuanza kazi.

Miradi ya Barabara Itakayojengwa kwa Utaratibu wa EPC+F

23. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/23 Wizara ilianza taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata Makandarasi wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara saba (7) zenye jumla ya kilometa 2035 kwa kutumia utaratibu wa Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC + F). Barabara hizi zitafungua fursa za kiuchumi katika maeneo zinapopita na kwa Taifa kwa ujumla.

Hatua iliyofikiwa hadi sasa ni kuwa Makandarasi wa miradi yote saba (7) wamepatikana na mikataba ya kazi za ujenzi inatarajiwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2023. Barabara ambazo zitajengwa kwa utaratibu huu wa EPC + F ni: -

i). Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo – Lumecha/Songea (km 435);
ii). Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (Simiyu) (km 339);
iii). Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboroti – Mrijochini – Dalai – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 460);
iv). Barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa Junction (km 453.42);
v). Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale (km 175);
vi). Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma (km 218) pamoja na barabara ya mchepuo ya Uyole – Songwe yenye urefu wa kilometa 48.9, na
vii). Barabara ya Mafinga – Mtwango – Mgololo (km 81).

24. Mheshimiwa Spika, hii ni mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu kuwa na miradi mikubwa yenye jumla ya kilometa 2,035 ambayo itaanza kutekelezwa kwa wakati mmoja katika maeneo mbalimbali nchini na itagharimu zaidi ya Shilingi Trilioni 3.7.

25. Mhe. Spika haya ni maoni na maelekezo ya Mhe. Dr. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Mungano wa Tanzania kwa ya kutaka kuifungu nchi kwa haraka sana. Munamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mradi ya Barabara Itakayotekelezwa kwa Utaratibu wa PPP

26. Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara kwa kutumia utaratibu wa kushirikisha Sekta Binafsi (Public Private Partnership - PPP), Wizara inaendelea na manunuzi ya makandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Expressway kutoka Kibaha – Chalinze – Morogoro yenye urefu wa kilometa 205.

Hadi sasa kazi inayoendelea ni uchambuzi (evaluation) wa Makandarasi walioonesha nia (Expression of Interest) ya kutekeleza mradi huu kwa sehemu ya kutoka Kibaha – Chalinze yenye urefu wa kilometa 78.9. Kwa sehemu ya Chalinze – Morogoro yenye urefu wa kilometa 126.1, Mshauri Elekezi anaendelea na kazi ya Upembuzi Yakinifu.

27. Mheshimiwa Spika, hii itakuwa ni mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu kuwa na mradi mkubwa hapa nchini ambao utatekelezwa kwa utaratibu wa PPP.

(Utekelezaji wa miradi ya Barabara na Madaraja umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 7 hadi 43)

Viwanja vya Ndege,

28. Mheshimiwa Spika, TANROADS imeendelea kutekeleza miradi ya uendelezaji wa viwanja vya ndege, ambapo ukarabati na upanuzi wa Viwanja vya Ndege vya Songea na Mtwara umekamilika. Aidha, kazi za ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege pamoja na eneo la usalama (Runway End Safety Area–RESA), usimikaji wa taa za usalama na taa za kuongozea ndege (AGL) katika Kiwanja cha Ndege cha Songwe zimekamilika. Kwa sasa, Mkandarasi anaendelea na kazi ya kumalizia ujenzi wa jengo la abiria ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 98.

29. Mheshimiwa Spika, Kazi ya ukarabati na upanuzi wa Viwanja vya Ndege vya Sumbawanga, Shinyanga, Tabora na Kigoma umeanza na Makandarasi wako kwenye hatua za maandalizi (mobilization).

30. Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, hadi Aprili, 2023 utekelezaji wa Package I unaohusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege (runway), barabara za maungio (taxiway), maegesho ya ndege (apron), uzio wa usalama, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani (access roads), maegesho ya magari (car parking) na usimikaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege (AGL) umefikia asilimia 18. Aidha, utekelezaji wa Package II unaohusisha ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, kituo cha zimamoto, kituo cha hali ya hewa na vituo vidogo nane (8) vya kufua umeme unaendelea na umefikia asilimia 2. Kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Musoma, kazi ya upanuzi na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege, maegesho ya ndege, barabara ya kiungio na uzio wa usalama inaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 47.

**Utekelezaji wa miradi ya Viwanja vya Ndege UMEONESHWA kuanzia ukurasa wa 51 hadi 54.**

31. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) iliendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa VIVUKO na maegesho ya vivuko katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utekelezaji wa kina wa miradi ya ukarabati, ununuzi na ujenzi wa vivuko, hadi Aprili, 2023, umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 45 hadi 47.

32. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2022/23.

Utekelezaji wa kina wa MIRADI WA Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 47 hadi 49.

32. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2023 utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Ujenzi: kuanzia Bodi ya Mfuko wa Barabara, Wakala ya Majengo Tanzania, Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadsiriaji Majenzi, Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Baraza la Taifa la Ujenzi, Kituo cha Usambazaji wa Tecknoloji Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 54 hadi 67

**B-2: SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU - 62)**

**Bajeti iliyoidhinishwa na fedha zilizotolewa kwa mwaka 2022/23**

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

33. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/23, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa Shilingi Bilion 94.546 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya Shilingi Bilion 71.955 sawa na asilimia 76.11 zilikuwa zimetolewa.

**Bajeti ya Maendeleo**

34. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/23, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa Shilingi Trilioni 2.041 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya Shilingi Trilioni 1.847 sawa na asilimia 90.51 zilikuwa zimetolewa.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA UTOAJI HUDUMA**

**Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya Barabara**

35. Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Usafiri wa Barabara unatekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA). Mamlaka hiyo inadhibiti utoaji wa huduma za usafiri wa kibiashara kwa abiria na mizigo ikijumuisha mabasi, malori, teksi, pikipiki za magurudumu matatu na za magurudumu mawili.

(Utendaji wa udhibiti wa usafiri kwa njia ya barabara umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu katika ukurasa wa 69 hadi 74).

**Huduma za Usafiri kwa Njia ya Reli**

**Shirika la Reli Tanzania (TRC)**

36. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara inaendelea na ujenzi wa Awamu ya Kwanza ya mradi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Standard Gauge kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza (Km 1,219) uliogawanyika katika vipande vitano (5). Hadi kufikia Aprili, 2023 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (Km 300) ni asilimia 98.14; Morogoro - Makutupora (Km 422) asilimia 93.83; Mwanza - Isaka (Km 341) asilimia 31.07; Makutupora - Tabora (Km 368) asilimia 7; na Tabora - Isaka (Km 165) asilimia 2.39.

37. Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya mwaka 2022/23, tuliahidi kuanza maandalizi ya ujenzi wa awamu ya pili ya reli ya Standard Gauge (SGR). Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, Serikali imeanza ujenzi wa Reli ya SGR kwa awamu ya pili katika kipande cha Tabora – Kigoma (Km 506) ambapo imesaini mkataba na Kampuni ya CCECC na CRCC kutoka China na kwa sasa Mkandarasi anakamilisha maandalizi ya ujenzi. Utendaji na Utekelezaji wa miradi ya reli kupitia TRC umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 74 hadi 78).

**Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**

38. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), hadi kufikia Aprili 2023, TAZARA ilisafirisha jumla ya tani 244,492 za mizigo na jumla ya abiria 765,706 wa njia ndefu. Utendaji wa TAZARA umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 78 hadi 80.

**Udhibiti wa Huduma za Usafiri kwa njia ya Maji**

39. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) imeendelea kusimamia ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri kwa njia ya maji na kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za usafiri majini.

40. Mheshimiwa Spika, TASAC inaendelea kusimamia ujenzi wa Kituo kikuu cha Uratibu wa shughuli za Utafutaji na Uokoaji cha kikanda kitakachojengwa eneo la Ilemela Mwanza.

Kwa sasa Mkandarasi tayari amekabidhiwa eneo kwa ajili ya kuanza shughuli za ujenzi na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi kumi na nane (18). Vilevile, mkandarasi amepatikana kwa ajili ya kujenga vituo vingine vidogo 3 vya utafutaji na uokoaji katika maeneo ya Kanyala (Geita), Nansio (Ukerewe) na Musoma (Mara) na kwa sasa maandalizi ya ujenzi yanaendelea. Utendaji wa udhibiti wa huduma za usafiri kwa njia ya maji na utekelezaji wa miradi umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 80 hadi 84.

**Huduma za Uchukuzi Katika Maziwa Makuu**

41. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) imeendelea kutoa huduma za usafiri na usafirishaji kwenye Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Hadi Aprili, 2023 MSCL ilisafirisha abiria 170,137 na tani za mizigo 18,909.

42. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa meli zinazotoa huduma katika Maziwa Makuu. Hadi Aprili, 2023 ujenzi wa meli mpya ya MV. Mwanza ulifikia asilimia 83; Ukarabati wa meli ya MV Umoja ulifikia asilimia 75.8 na Ukarabati wa MT Sangara ulifikia asilimia 90.7.

Aidha, Serikali kupitia MSCL ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na Mkandarasi ili kuwezesha kuanza ujenzi wa meli mbili (2) katika Ziwa Tanganyika; Meli moja (1) katika Ziwa Victoria na Chelezo katika Ziwa Tanganyika.

Hatua iliyofikiwa ya ukarabati ya MV Liemba hadi sasa ni kuwa





Makandarasi amepatikana na mkataba ya kazi za ukarabati wa meli hiyo inatarajiwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2023. Kazi ukarabati itafanyika kwa miezi tisa (9). Pia, kazi ya matengenezo ya utulivu (stability) ya MV Muongoza itaanza hivi karibuni. Utendaji na utekelezaji wa miradi MSCL umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 85 hadi 87).

**Huduma za Bandari**

43. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2023 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) ilihudumia shehena ya tani milioni 20.851 na makasha 765,504. Aidha, TPA inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Bandari za Mwambao na za Maziwa Makuu. Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam imefikia asilimia 96. Aidha, kwa Bandari ya Tanga, TPA imekamilisha Awamu ya Pili ya Uboreshaji wa Bandari hiyo kwa kuimarisha na kuboresha Gati Na. 1 na 2 zenye urefu wa mita 450 ambapo mradi umekamilika kwa asilimia 99. Kwa upande wa Bandari za Maziwa makuu, ujenzi wa Bandari ya Karema umekamilika na imeanza kutumika. Aidha, ujenzi wa gati, ghala la kuhifadhia makaa ya mawe, jengo la abiria, ofisi na sehemu ya kuegesha meli (ramp) katika Bandari ya Ndumbi Ziwa Nyasa umekamilika. Utendaji na utekelezaji wa miradi ya TPA umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 87 hadi 95.

**Udhibiti wa Huduma za Usafiri kwa Njia ya Anga**

44. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imeendelea kutoa huduma za udhibiti wa usafiri wa anga, viwanja vya ndege, masuala ya kiusalama na kiuchumi katika huduma za usafiri wa anga pamoja na kutoa huduma za uongozaji ndege katika viwanja 14 nchini. Utendaji na utekelezaji wa miradi ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga unaonyeshwa katika kitabu cba hutuba ya bujeti kuanzia ukurasa wa 95 hadi 100.

**Huduma za Viwanja vya Ndege**

45. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) ina jukumu la kusimamia, kuendesha, kuboresha na kuendeleza viwanja vya ndege 58 vinavyomilikiwa na Serikali.

46. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TAA imekamilisha maandalizi ya mahitaji ya kiufundi na ununuzi wa kandarasi kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya abiria katika viwanja vya ndege vya Mpanda, Songea, na Kahama. Pia. imeanza maandalizi ya ujenze wa Jengo la Waongoza Ndege katika Kiwanja cha Ndege Bukoba. Pia TAA imeanza matayarisho ya ukamilisha wa ujenzi wa Jengo la Abiria wa Kiwanja cha ndege cha Mwanza.

47. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2023, kazi ya uwekaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma ili kiweze kutumika kwa saa 24 imefikia asilimia 40.

48. Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa urejeshaji wa shughuli za uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) chini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Wizara inaendelea na taratibu za kutunga Sheria mahsusi ya TAA kwa ajili ya kuwezesha Viwanja vyote vya Ndege nchini, ikiwemo KIA, kuwa chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Tanzania. Utekelezaji wa majuku ya Viwanja vya Ndege umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 101 hadi 107.

**Huduma za Usafiri kwa Njia ya Anga**

49. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na juhudi za kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL). Juhudi hizo ni pamoja na kuendelea na usimamizi wa utengenezaji wa ndege mpya nne (4) ambazo ni Boeing 767-300F moja (1) ya mizigo inayotarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwezi Mei, 2023; Ndege 2 za Boeing 737-9 zinazotarajiwa kuwasili mwezi Agosti na Disemba, 2023; na Ndege 1 ya Boeing 787-8 Dreamliner inayotarajiwa kuwasili mwezi Februari, 2024. Kutokana na mpango wa Serikali wa kuongeza ndege mpya nne (4), ATCL inatarajia kupanua wigo wa safari zake kwa kuongeza vituo vipya sita (6) vya nje na 3 vya ndani.

Utendaji wa utoaji huduma za usafiri na Usafirishaji kwa njia ya anga umeainishwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 107 hadi 110.

**HUDUMA ZA HALI YA HEWA**

50. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeendelea kutekeleza mradi wa kununua na kufunga Rada nne (4) za hali ya hewa. Rada mbili (2) tayari zimeshapokelewa na kazi ya ufungaji inaendelea katika mikoa ya Mbeya na Kigoma na Rada nyingine mbili (2) zitakazofungwa mkoani Dodoma na Kilimanjaro zinatarajiwa kuwasili mapema mwakani. Utendaji na utekelezaji wa miradi ya huduma za hali ya hewa umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 111 hadi 113.

**TAASISI ZA MAFUNZO**

51. Mheshimiwa Spika, Utendaji WA Taasisi za Mafunzo zilizo chini ya WIZARA (sekta ya Uchukuzi) umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 113 hadi 121.

**C. CHANGAMOTO ZILIZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA**

52. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imekabiliwa na changamoto mbalilimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Changamoto hizo na mikakati ya kuzitatua zimeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 137 hadi ukurasa wa 142.

**D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

53. Mheshimiwa Spika, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2023/24 umeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 pamoja na maelekezo ya Serikali. Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Sekta ya Ujenzi na Sekta ya Uchukuzi ni kama ifuatavyo:-

**D – 1: SEKTA YA UJENZI (FUNGU – 98)**

Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

54. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/24, Sekta ya Ujenzi imetengewa Shilingi Bilion 48.395 ikiwa ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka 2023/24 ni Shilingi Trilion 1.419. Kati ya fedha hizo, Shilingi Trilion 1.084 ni fedha za ndani na Shilingi Bilion 335.176 ni za fedha za nje. Kati ya fedha za ndani Shilingi Bilion 599.756 ni fedha kutoka Mfuko wa Barabara na fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni Shilingi Bilioni 484.909.

Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika Kiambatisho Na. 1 na Na. 2.

55. Mheshimiwa Spika, VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI YA SEKTA YA UJENZI

(i) Kuanza ujenzi wa miradi saba (7) ya barabara yenye jumla ya kilometa 2,035 kwa kutumia utaratibu wa Engineeering Procurement Construction and Finance ( EPC + F).
(ii) Kuanza utekelezaji wa ujenzi wa barabara kutoka Kibaha – Chalinze – Morogoro Expressway yenye urefu wa kilometa 205 kwa kutumia utaratibu wa kushirikisha Sekta Binafsi (Public Private Partnership - PPP).
(iii) Kuendelea na ujenzi wa miradi mikubwa ya barabara katika maeneo mbalimbali yenye jumla ya urefu wa kilometa 1,031.98.
(iv) Kuendelea na Miradi ya Ujenzi wa Barabara iliyosaniwa Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 yenye jumla ya urefu wa kilometa 393.6
(v) Kuendelea na ujenzi wa madaraja makubwa mawili (2) ya JPM (Kigongo – Busisi, Mwanza) na Pangani (Tanga) pamoja na kujenga madaraja mengine katika maeneo mbalimbali nchini.
(vi) Kuanza utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara zenye jumla ya urefu wa kilometa 269.12 ambazo zinatarajiwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2022/23.
(vii) Kuendelea na utekelezaji wa mradi ujenzi wa uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Msalato pamoja na Kuendelea na kazi za ukarabati na upanuzi wa viwanja vingine vya ndege katika mikoa mbalimbali.

56. Mheshimiwa Spika, Miradi yote hiyo ya barabara na madaraja ikamilika itakuwa na jumla ya kilometa 3,934.7 za barabara zilizojengwa kwa lami ambazo zitaongeza urefu wa mtandao wa barabara za lami zilizopo sasa za kilometa 11,587.82 na kufikia kilometa 15,522.52 ambalo ni sawa na ongezeko la asilimia 34.

**D - 2: SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU – 62)**

**Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo**

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/24, Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) imetengewa jumla ya Shilingi Trilioni 2.086 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 118.215 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi Trilioni 1.968 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha imeovyooneshwa katika Kiambatisho Na. 6.

58. Mheshimiwa Spika, VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI YA SEKTA YA UJENZI

i. Mradi wa Kuwezesha Taasisi (Institutional Support) – Shilingi bilioni 18.3;
ii. Mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Usafiri katika Ziwa Victoria – Shilingi bilioni 1.73;
iii. Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam – Shilingi bilioni 93.80.
iv. Miradi inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Reli (RIF)– Shilingi bilioni 294.80;
v. Mradi wa Ukarabati wa Njia Kuu ya Reli Iliyopo (MGR) – Mradi wa Tanzania Intermodal Railway II – Shilingi bilioni 11.72;
vi. Mradi wa Ujenzi wa Reli Mpya ya Standard Gauge – Shilingi trilioni 1.113;
vii. Mradi wa Ununuzi wa Rada, Vifaa na Ujenzi wa Miundombinu ya Hali ya Hewa – Shilingi bilioni 13.00;
viii. Mradi wa Uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) – Shilingi bilioni 300.00;
ix. Mradi wa Ujenzi wa Meli Mpya na Ukarabati wa Meli – Shilingi bilioni 100.00;
x. Mradi wa Kuboresha Miundombinu na Ununuzi wa Vifaa vya Kufundishia – Shilingi bilioni 2.27;
xi. Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya TAZARA– Shilingi bilioni 13.19; na
xii. Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya Kuongozea Ndege na Uendelezaji wa Chuo cha Mafunzo ya Usafiri wa Anga – Shilingi bilioni 6.5.

**E. SHUKRANI**

59. Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kuwapongeza na kutambua mchango mkubwa unaotolewa na viongozi wenzangu katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu, nikianzia na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya na Mheshimiwa Fred Mwakibete; Makatibu Wakuu, Balozi Mhandisi Aisha Salim Amour (Ujenzi) na Ndugu Gabriel Joseph Migire (Uchukuzi); Naibu Makatibu Wakuu Ndugu Ludovick James Nduhiye (Ujenzi) na Dkt. Ally Saleh Possi (Uchukuzi). Vilevile, kipekee napenda kuishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa jitihada zao katika utekelezaji wa Majukumu ya Wizara.

60. Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati na kuwatambua wadau wote wa Wizara ikiwa ni pamoja na Washirika mbalimbali wa Maendeleo ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa Programu, Miradi na Mipango mbalimbali ya Wizara. Aidha, napenda kuwatambua wafuatao: Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga, Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini, Shirika la Hali ya Hewa Duniani, UNESCO, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia, Japan (JICA), OPEC Fund, Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Ujerumani (KfW), Shirika la Maendeleo la Ufaransa, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Shirika la Maendeleo la Marekani, Kuwait (KFAED), HSBC, TMEA, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, Dubai, China, Denmark, Norway, Ubelgiji, Ujerumani na Uturuki, Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi za fedha zote za kifedha nchini na Asasi mbalimbali zisizokuwa za Serikali; Sekta Binafsi pamoja na wadau wengine wengi ambao sitamaliza endapo nitawataja wote.

61. Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi Mhe. Naibu Spika na kwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (www.mwt.go.tz).

**F MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

62. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 3,554,783,957,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,468,238,449,000.00 ni kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi na Shilingi 2,086,545,508,000.00 ni kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

**SEKTA YA UJENZI (FUNGU 98)**

63. Mheshimiwa Spika, Shilingi 1,468,238,449,000.00 za Fungu 98 (Ujenzi) zinajumuisha Shilingi 48,395,392,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 1,419,843,057,000.00 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

**SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU 62)**

64. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uchukuzi inaombewa jumla ya Shilingi 2,086,545,508,000.00. Kati ya hizo, Shilingi 118,215,599,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 1,968,329,909,000.00 ni kwa ajlili ya Miradi ya Maendeleo.

65. Mheshimiwa Spika, pamoja na Hotuba hii, nimeambatisha Miradi ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/24 kuanzia Kiambatisho Na. 1 – 6. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.



## TANROADS yatangaza zabuni ujenzi wa daraja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) umetangaza zabuni kwa ajili ya kujenga upya Daraja la Kalema Maziwani linalounganisha Wilaya ya Kiteto, Chemba na Kondoa lililosombwa na mvua mwaka 2019.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Chemba (CCM), Mohamed Monni na kusema zabuni hizo zimepangwa kufunguliwa Juni 5, mwaka huu.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itajenga daraja hilo.

Akijibu swali hilo, Kasekenya alisema serikali kupitia wakala huo tayari imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kujenga upya Daraja la Kalema Maziwani katika Barabara ya Kondoa – Bicha – Dalai ambalo lilitita kutokana na mvua kubwa za mwaka 2019.

Alisema: "Ili kujenga daraja hilo Mei 19 mwaka huu Wakala wa Barabara Tanzania imetangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi na zabuni hizo zimepangwa kufunguliwa tarehe 5 Juni, 2023".

# Wananchi 10,000 wajengewa uwezo wa kujua haki zao

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

**Wananchi wenye kipato cha chini waliokuwa wakishindwa kupata huduma zote muhimu zinazohusu ukatili na kuacha haki zao kupotea kwa kushindwa kuzifikia huduma.**

WANANCHI 10,000 kutoka mikoa ya Singida na Shinyanga wamejengewa uwezo wa kujua haki zao na kuwezeshwa kiuchumi ili kukabiliana na matukio ya ukatili wa kijinsia.

Elimu hiyo imetolewa na Umoja wa Mataifa (UN) kupitia mashirika yake ambayo ni linaloshughulikia Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), linaloshughulikia masuala ya wanawake (UN Women) kupitia programu ya pamoja ya kutambua usawa wa kijinsia.

Msaidizi wa Mwakilishi Mkaazi wa UNFPA Tanzania, Dk. Majaliwa Marwa, aliyasema hayo jana kwenye uzinduzi wa vituo vya huduma shufaa katika Hospitali ya Wilaya ya Ikungi na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida.

Alisema vituo hivyo vimejengwa kupitia programu hiyo inayotekelezwa na mashirika ya UNFPA na UN Women kwa ufadhili wa Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA) ili kuwahudumia waathirika waliofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Dk. Marwa alisema programu hiyo ni ya miaka mitatu, inalenga kuleta usawa wa kijinsia, kukomesha ukatili na mila potofu dhidi ya wanawake na watoto na kupunguza umaskini kwa kuboresha hali ya kiuchumi kwa wanawake na kuimarisha mipango ya matumizi ya ardhi kijiji.

"Programu ya uwezeshaji wa kiuchumi inayotekelezwa na UN Women imeonyesha matukio chanya ambapo kituo cha ukusanyaji mazao katika Wilaya ya Ikungi kinawawezesha wakulima wadogo wanawake wanaouza mazao ya bustani kukusanya na kuhifadhi mazao yao," alisema.

Aidha, alisema UNFPA imeimarisha uwezo wa taasisi za ndani kwa watoa huduma kwenye vituo hivyo na wahudumu wa afya zaidi ya 450, wasaidizi wa kisheria, maofisa wa polisi wamepewa mafunzo ya jinsia ya kuzuia na kukabiliana na ukatili wa kijinsia.

Naibu Mkurugenzi wa KOICA, Heo Eun alisema wanawake na watoto wamekuwa ni sehemu ya mipango na vipaumbele vya shirika hilo katika utendaji kazi kwa kuwasaidia kuboresha uchumi wao.

Alisema KOICA kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania wataendelea kushirikiana katika kuendeleza jitihada za kuwainua wanawake kiuchumi hasa ikizingatia kuwa uchumi ukiimarika kwa jamii hiyo hata matukio ya unyanyasaji wa kijinsia hayatakuwapo.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo, Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Thomas Apson, alisema kufunguliwa kwa vituo hivyo kutasaidia hasa ikizingatia kuwa matukio ya ukatili yamezidi kujitokeza katika jamii.

Alisema wananchi wenye kipato cha chini waliokuwa wakishindwa kupata huduma zote muhimu zinazohusu ukatili na kuacha haki zao kupotea kwa kushindwa kuzifikia huduma.

"Kituo hiki sasa ni suluhisho maana huduma zote za kitabibu na za kisheria zitapatikana eneo moja, nitoe rai kwa wananchi kutumia kituo hiki pindi matukio ya ukatili yanapotokea ili yatolewe taarifa kwa wakati na haki ya mwathirika wa ukatili ipatikane kwa wakati," alisema.



Mkazi wa Kijiji cha Ndogowe, Kata ya Nghambaku wilayani Chamwino, Kedmond Michael (kulia), akizungumza na waandishi wa habari juzi, kwa niaba ya wanakijiji wenzake wakati wakitoa malalamiko dhidi ya uongozi wa kijiji hicho kutoitisha mikutano ya hadhara ya kuwasomea mapato na matumizi kwa mujibu wa sheria kwa kipindi kirefu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# DC ahimiza utoaji taarifa vitendo ukatili kijinsia

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Mwema, ameitaka jamii kutofumbia macho vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto badala yake watoe taarifa ili hatua kali za kisheria zichukuliwe.

Alitoa kauli hiyo juzi kwenye hafla ya kugawa vyeti vya kuzaliwa 446 kwa watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu vilivyotolewa na Shirika la World Vision Tanzania mkoani Dodoma.

Alisema wananchi wanapaswa kushirikiana na serikali kwa ajili ya kutoa taarifa ya vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyofanywa kwenye jamii kutokana na imani zao za kishirikina na kukatisha ndoto za watoto.

"Naomba wananchi mwendelee kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi pale mnaposikia kuna tukio lolote la ukatili limefanyika," alisema Mwema.

Alisema serikali imekuwa ikipiga vita vitendo vya ukatili na wananchi wanapaswa kutoa ushirikiano ili kukomesha ukatili huo.

"Nimefurahi kuona shirika lisilo la kiserikali la World Vision wanaunga mkono jitihada za kupinga ukatili wa kijinsia wananchi mnapaswa kutoa ushirikiano pale mnapotakiwa kutoa taarifa zenye viashiria vya ukatili wa kijinsia," alisema.

Meneja wa Kanda ya Kati wa World Vision Tanzania, Pudensiana Rwezaura, alisema wanatarajia kusaidia watoto milioni 3.2 ifikapo mwaka 2025 ili kuhakikisha watoto wote wanakuwa na vyeti vya kuzaliwa.

Rwezaura alisema wanafanya hivyo kupitia mradi wa Kongwa AP ambao unaotekelezwa ndani ya miaka mitano katika Wilaya ya Kongwa.

Alisema mpaka sasa tayari wamegawa vyeti vya kuzaliwa katika vijiji vya Mnuku, Mvurungo, Mkoka, Mlanje, Makawa na Muungano huku akisisitiza wazazi kujenga utaratibu wa kuwa na vyeti vya kuzaliwa vya watoto kwa sababu vina umuhimu mkubwa.

Alisema wanafanya hivyo ili kugusa ustawi wa watoto moja kwa moja hususani waliopo kwenye mazingira magumu.



# Waingiwa hofu maeneo yao kuzungushiwa ukuta

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANANCHI wa Sae na Ituha jijini Mbeya wameingiwa na taharuki baada ya watu wanaodaiwa kuwa wamepewa kandarasi ya kujenga uzio kuzunguka eneo la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole kuingia katika maeneo yao na kufyeka mazao ili kupitisha mpaka.

Wananchi hao walisema wameshangazwa na kitendo hicho kwa kuwa eneo hilo ambalo linataka kuzungushiwa uzio tayari walisharejeshewa na serikali kupitia aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Mtaa wa Ituha, Elias Mwakyusa, alisema kuwa awali kulikuwa na mgogoro katika eneo hilo baina yao na TARI Kituo cha Uyole baada ya taasisi hiyo kushindwa kuwalipa wananchi fidia ili walichukue.

Alisema baada ya malalamiko ya muda mrefu bila mafanikio, wananchi walifikisha suala hilo kwa mbunge wao ambaye ni Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson ambaye aliwasaidia kufikisha kilio hicho serikalini.

**Nimeshamwelekeza Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, kuwaita wote wanaohusika na mgogoro huo ili akae nao na kuwasikiliza ili hatua za kumaliza suala hilo ziweze kuchukuliwa.**

Alisema kuwa juzi mbunge wao alimleta Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi ambaye alimaliza mgogoro huo kwa kuamuru eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 67 lirejeshwe kwa wananchi.

Alisema baada ya kutolewa uamuzi huo, wananchi walianza kuliendeleza kwa kujenga nyumba na kulima mazao, wakiamini kuwa mgogoro umemalizika na sasa ardhi hiyo ni mali yao halali.

"Tunashangaa kuona tena eneo hili ambalo tulisharejeshewa na serikali linataka kuchukuliwa tena na kilimo, waliokuja kujenga uzio wamefyeka mazao yetu na eneo ambali wanataka kupitisha mpaka, wanazingira nyumba nyingi za wananchi, tunaomba serikali iingilie kati suala hili," alisema Mwakyusa.

Baadhi ya wananchi ambao wamezungumzia suala hilo walisema kuwa wanamini ardhi hiyo ni mali yao halali ambayo waliachiwa na wazazi wao, hivyo hawako tayari kuiachia kwa vile tayari wameshaanza kuiendeleza.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alikiri kuutambua mgogoro huo na kudai kuwa tayari ameshatoa maelekezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Benno Malisa kushughulikia.

"Nimeshamwelekeza Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, kuwaita wote wanaohusika na mgogoro huo ili akae nao na kuwasikiliza ili hatua za kumaliza suala hilo ziweze kuchukuliwa," alisema Homera.

Alisema baada ya kusikiliza pande zote zinazohusika na suala hilo ndipo ofisi yake itajua hatua sahihi za kuchukua na kumaliza mgogoro huo ili wananchi waishi kwa amani.



Mkufunzi wa Shirika la Uwezo, Anyimike Hezron (kushoto), akigawa majarida ya tathmini ya utafiti wa stadi za maisha na maadili kwa watoto wenye umri wa kuanzia miaka 13 hadi 17, wilayani Mbozi mkoani Songwe juzi, uliokuwa na lengo la kutoa elimu ya namna gani watoto wanaweza kukua kwa kuzingatia maadili, kujiamini na uwezo wa kushughulikia masuala mbalimbali katika jamii. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Ujenzi mnada wa mifugo Kata ya Utengule waanza

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imeanza kujenga mnada mkubwa wa mifugo katika Kata ya Utengule Usangu wilayani Mbarali Mkoa wa Mbeya kwa lengo la kuwasaidia wafugaji kupata soko la uhakika.

Mradi wa ujenzi wa mnada huo utagharimu zaidi ya Sh. milioni 500 ambazo zimetolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Diwani wa Kata ya Utengule Usangu, Samora Msosa, aliyasema hayo jana na kwamba mradi huo pia utahusisha ujenzi wa josho la kuogesha mifugo na kituo maalum cha kutolea tiba na elimu ya ufugaji kwa wananchi.

Alisema mradi huo pia utatumika kama soko la bidhaa nyingine za viwandani na hata mazao ya wakulima.

"Serikali imetuletea mradi mkubwa wa ujenzi wa mnada ambao utakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi wangu, tutautumia kuuza mifugo yetu na bidhaa zitokanazo na mifugo kama vile maziwa, nyama na ngozi, lakini hata wakulima watauza mazao yao na bidhaa nyingine za viwandani," alisema Msosa.

Alisema kuwa mradi huo tayari ulishaanza kutekelezwa kwa kujenga uzio kuzunguka eneo la mnada, ambapo pia josho na baadhi ya majengo ya ofisi tayari yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Alisema mradi huo ukikamilika utakuwa mkombozi kwa wananchi wa Kata ya Utengule - Usangu na maeneo ya jirani kwa kupata eneo zuri la kufanyia biashara.

Aidha, alisema kuwa mradi huo pia utakuwa chanzo kizuri cha mapato cha Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ambao pia watakusanya ushuru kutokana na biashara itakayokuwa ikifanyika mahali hapo.

# Watumishi 13 halmashauri wahojiwa tuhuma ubadhirifu

**Na Grace Mwakalinga,** TUNDUMA

JESHI la Polisi linawahoji watumishi 13 wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, mkoani Songwe kwa tuhuma za kuhusika na ubadhirifu wa fedha za miradi.

Akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo juzi, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Philemon Magesa, alisema watumishi hao wamefanya ubadhirifu, wizi wa vifaa vya ujenzi na usimamizi mbovu wa ujenzi wa miradi ya maendeleo.

Alisema makosa hayo yalifanyika katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020 hadi mwaka huu walipobainika na kuanza kuchukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria.

Aliwataja watumishi hao kuwa ni Japhet Chota anayedaiwa kuhusika katika wizi vifaa ujenzi wa Stendi Kuu ya Mabasi Mpemba, Pendo Sechambo, anayetuhumiwa kwa kosa la usimamizi mbovu wa mradi wa ujenzi wa dampo la Namole na Rafael Simkonda anayedaiwa kuhusika katika ubadhirifu wa fedha katika ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mwaka kati.

Wengine ni Josephat Kayombo ambaye ni Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu akituhumiwa kuhusika katika wizi wa vifaa vya ujenzi wa Stendi Tunduma ikiwamo saruji na rangi anavyodaiwa kuvichukua na kwenda kujengea nyumba yake, Dk. Enock Mwambalaswa, ambaye ni Mkuu wa Divisheni ya Afya ya Jamii na Huduma za Lishe akituhumiwa kwa usimamizi hafifu wa miradi na kutokuwa na taarifa kina za ujenzi wa Zahanati ya Makambini.

Magesa aliendelea kuwataja watumishi wengine wanaohojiwa kuwa ni Wakili Frank Sikalengo anayetuhumiwa kughushi mikataba ya ujenzi, Obed Mwakalinga ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Ugavi na Manunuzi anayehusishwa na ubadhirifu fedha za miradi, Ibrahim Lulimo ambaye ni Ofisa Ugavi akituhumiwa kununua vifaa hewa na Patricia Mbighili ambaye ni Ofisa Elimu Idara ya Sekondari akituhumiwa kuhujumu fedha za mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Dk. Samia.

Wengine ni Ally Farayo ambaye ni Mhandisi Daraja la Pili kwa tuhuma za kushindwa kusimamia matumizi ya vifaa vya ujenzi, Dickson Kisenime ambaye ni Mhandisi Daraja Pili akituhumiwa kwa ubadhirifu fedha za miradi kwa kufanya malipo hewa ya Sh. milioni 76 malipo kwa ajili ya mikataba ya halmashauri.

Alisema mtumishi mwingine, Albert Alphonce atalazimika kukatwa asilimia 10 ya mshahara wake kufidia fedha zilizopotea wakati wa ujenzi wa Kituo cha Afya Chapwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi wa Polisi, (ACP) Theopista Mallya alisema tayari Jeshi la Polisi limeshawakamata watuhumiwa hao na kuanza kuwahoji kulingana na tuhuma zinazowakabili.

## Serikali yatoa kongole ripoti stadi za maisha, maadili

**Na Renatha Msungu**

SERIKALI imeipongeza ripoti ya utafiti wa stadi za maisha na maadili iliolenga kubaini uwezo wa watoto kwenye saikolojia, hisia na akili inayotoa taswira ya kupunguza vitendo vya ukatili kwa watoto.

Utafiti huo ulifanywa na Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation, kwa kushirikiana na Zizi Afrique Foundation, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Uwezo Tanzania, Girls Livehood, Reginal Education learning Initative, Guluka Kwalala Youth and Environment Group na ulifanyika katika wilaya 34.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Tawala Mwandamizi wa Wilaya ya Ilala, Frola Mgonja kwa niaba ya Mkuu wa wilaya hiyo wakati wa uzinduzi wa ripoti hiyo.

Alisema ripoti hiyo itachochea kupunguza ukatili kwa watoto kwa sababu imeeleza namna ya watoto wanavyoweza kujikinga na masuala ya ukatili ikiwamo kupewa ujasiri wa kujitambua na kuwa na uwezo wa kujieleza.

"Watoto wakiwa na uwezo wa kujieleza kwa asilimia kubwa matatizo ya ukatili yatakoma kabisa kwa sababu watasaidia kuonyesha wahalifu wa vitendo hivyo," alisema Mgonja.

Alisema yale yaliyowasilishwa katika ripoti hiyo yachukuliwe na watunga sera, kwamba yasiishie kwenye machapisho badala yake yafanyiwe kazi.

Mkurugenzi wa Shirika la Guluka Kwalala Youth and Environment Group, Omary Ngalomba, alisema ripoti hiyo imeakisi mazingira halisi ya mtaani.

Ngalomba alisema shirika hilo ambalo ni kinara wa uandaaji wa ripoti hiyo limekuwa likifuatilia mazingira halisi ambayo watoto wanaishi na kusababisha kufanya utafiti huo kwa kushirikiana na mashirika mengine.

Mratibu wa mradi huo, George Pius, alisema utafiti uliofanywa katika kaya 336 za Wilaya ya Ilala umebaini vijana kuanzia miaka 13 hadi 17 baadhi yao hawawezi kufanya matumizi ya simu za kidijitali, huku asilimia 33 wanatumia kirahisi na asilimia 37 wanatumia kwa tabu.

# Ofisi ya Mufti kufanya utafiti ongezeko la talaka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISI ya Mufti Mkuu wa Zanzibar imeanza kufanya utafiti wa kujua sababu za ongezeko la talaka na njia ya kukabiliana nayo ambayo miongoni mwa waathirika wakubwa ni wanawake na watoto.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, wakati akifanya majumuisho ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2023/2024 na kujibu hoja za wajumbe wa baraza hilo waliotaka kufahamu sababu za kuwapo kwa wingi wa talaka.

Alisema serikali imeliona tatizo la kuwapo kwa wingi wa talaka na ndoa nyingi kuvunjika katika kipindi kifupi cha ndoa.

**Baadhi ya ndoa zinafungwa bila ya kufuata masharti ya ndoa ambayo ni ridhaa ya wazazi wawili au walii ambao ndiyo wahusika wakubwa.**

Alisema katika utafiti wa hatua ya kwanza imebainika wanandoa wengi wanaingia katika makubaliano ya ndoa bila ya kupata elimu ya ndoa na matokeo yake hawajui fursa na haki zinazopatikana katika ndoa.

Aidha, alisema baadhi ya ndoa zinafungwa bila ya kufuata masharti ya ndoa ambayo ni ridhaa ya wazazi wawili au walii ambao ndiyo wahusika wakubwa.

Waziri huyo alisema hatua zingine zilizochukuliwa na ofisi ya Mufti kwa sasa ni kuanzisha mafunzo kwa wanandoa watarajiwa na waliomo katika ndoa ambayo yatawawezesha kufahamu matatizo yaliyopo katika ndoa na namna ya kukubaliana nazo.

Harouna alisema tayari wanandoa watarajiwa 522 wamepata mafunzo ambayo yameanzishwa na ofisi ya Mufti katika kipindi cha miaka miwili ambapo lengo ni kuwawezesha kumudu ndoa na kuishi kwa amani na utulivu.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio mapato na matumizi ya bajeti hiyo, waliitaka wizara kukabiliana na tatizo la ongezeko la talaka kwa kufanyika utafiti wa kina kujua chanzo chake.

Mwakilishi wa Viti Maalumu, Bihindi Hamad Khamis, alisema kwa mujibu wa taarifa za ofisi ya Mufti zinazoonesha katika kipindi cha Julai mwaka 2022 hadi Machi 2023 jumla ya migogoro inayohusu talaka na ndoa 871 imeripotiwa.

Alisema wingi wa talaka hizo unahitaji kufanyiwa kazi kwa ofisi ya Mufti kuja na utafiti utakaobainisha na kujua sababu za ongezeko la talaka.




Mkurugenzi Mkuu wa Tigo, Kamal Okba (katikati), akipokea zawadi ya mlango wa Zanzibar kutoka kwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Mohamed Said, katika mkutano wa wadau wa sekta ya usafirishaji Kanda ya Mashariki, jijini Zanzibar jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Chama cha Mawakala wa Usafiri Afrika Mashariki (AE-SATA) Tanzania, Moustafa Khataw. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Asasi za kiraia zatoa mapendekezo kwa serikali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUTANO wa pili wa jukwaa la asasi za kiraia umemalizika visiwani Zanzibar kwa wajumbe kutoa mapendekezo kwa serikali kutambua mchango wa asasi za kiraia katika ripoti za maendeleo na kuondosha dhana ya kwamba asasi ni adui wa serikali.

Akitoa mapendekezo hayo Mwenyekiti wa mkutano huo, Hassan Khamis, alisema licha ya asasi kupata vibali kufanya utafiti lakini bado hazitumiwi katika shughuli za ndani na upangwaji wa shughuli za maendeleo.

Alisema ni wakati muafaka kwa serikali kutumia utafiti zinazofanywa katika utekelezaji wa maendeleo.

Khamis alisema ni muhimu serikali kuzishirikisha asasi za kiraia katika mabadiliko ya sheria katika ngazi ya uundwaji, utekelezaji na hatua ya utoaji wa ripoti pamoja na kuwa na mawasiliano mazuri.

Mwenyekiti huyo alisema bado kuna baadhi ya watendaji serikalini wanaendelea kuwa vikwazo kwa asasi za kiraia katika kutoa ushirikiano, hivyo ni muhimu serikali kutoa elimu kwa watumishi wote dhana ya uwepo wa asasi hizo.

Alisema pia bado kunatatizo la kisheria juu ya uendeshwaji wa asasi za kiraia, hivyo serikali iangalie baina ya asasi zinazoingiza faida na zisizoingiza faida kwa sababu asasi hutegemea wadau na wafadhili kutekeleza shughuli ambazo zinasaidia serikali.

"Tunaomba sheria kandamizi za kodi ziangaliwe upya kwa sababu zinadumaza asasi za kiraia katika kuisaidia jamii hasa ikizingatiwa kuwa asasi nyingi zinatatizo la kifedha," alisema.

Aidha, alisema asasi nyingi bado zipo nyuma katika utumiaji wa teknolojia ambako kuna fursa nyingi, hivyo ni vyema kuelewa fursa za kidijitali ili kuzalisha fedha za uendeshaji wa asasi na uelimishaji jamii.

Akifunga mkutano huo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara za SMZ, Mikidadi Mzee, alizitaka asasi za kiraia kuitumia fursa waliyopewa na kuaminiwa na serikali ikiwamo kupewa usajili.

Alisema serikali itaendeleza kudumisha ushirikiano na asasi za kiraia na kuweka mazingira wezeshi ili kufanya kazi zao kwa ufanisi.

"Mimi ni muumini wa asasi za kiraia, faida ya uwepo wa asasi hizi ipo, lakini tuhakikishe malengo yetu yanaweza kufikiwa hivyo tuongeze ushirikiano kwa wananchi, serikali na wafadhili," alisema.

Aidha aliwataka wana asasi hao kuwa waadilifu, kufuata tamaduni za nchi na kuhakikisha wanaheshimu tamaduni za jamii husika na kwamba serikali haiko tayari kuona asasi hizo zinapotosha jamii.

Alisema serikali inazifuatilia asasi zote za kiraia kwa sababu kuna viashiria kwa baadhi ya asasi za kiraia Tanzania zinatuhumiwa kujihusisha na vitendo vya udhalilishaji na ukiukwaji wa maadili ya nchi.

Pia alizitaka asasi hizo zinapotoa elimu kwa jamii kuhusu masuala mbalimbali kuzingatia amani na utulivu wa nchi.

Mkutano huo wa siku tatu ulizikutanisha asasi za kiraia 250 kutoka Zanzibar na Tanzania Bara na kufunguliwa na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**REGISTRATION OF DOCUMENTS ORDINANCE**
**(CAP 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

**THIS CHANGE OF NAME DEED** is made this 30th day of August, 2018 by me **GRACE WILLIAM SIWITI**, formerly known as **GRACE LIKOKOLA,** of Post Office Box Number 41352, a resident of **TABATA SEGEREA, ILALA** – Dar es salaam.

**WITNESSES AND IT IS HEREBY DECLARED** as follows:

- I absolutely renounce and abandon the use of my said former names of **GRACE LIKOKOLA,** and I assume and determine to take and use the new name **GRACE WILLIAM SIWITI** in substation of my former names of **GRACE LIKOKOLA.**
- **AND IN PURSUANCE** of such change of names(s) as aforesaid **I DECLARE I** shall at all times hereafter in all records, documents and other writings and in all actions and dealings and on all occasions whatsoever use the new name of **GRACE WILLIAM SIWITI** in substitution for my former names of **GRACE LIKOKOLA** so relinquished as aforesaid former names, but by the new name of **GRACE WILLIAM SIWITI** only.
- **AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUIRE** all person at all times to describe and address me by the new name of **GRACE WILLIAM SIWITI.**

**IN WITNESS** whereof I have hereunto subscribe my new name of **GRACE WILLIAM SIWITI,** and have affixed my signature the day and year herein written.

SIGNED and DELIVERED by the said GRACE WILLIAM SIWITI introduced to me by ______ the later known to me personally in my presence this 30th day of August, 2018

BEFORE ME:

COMMISSIONER FOR OATHS

DEPONENT



**IN THE DISTRICT COURT OF ILALA**
**AT KINYEREZI**
**MIS CIVIL APPEAL CASE, MATR CAUSE REV, PROB ADMN. CAUSE NO. 19/2022**
**DR. GEOFREY ONESMO MASSAWE**
**PLAINTIFF/APPELLANT/APPLICANTAPPLICANT**
**VERSUS**
**JOSEPH BONIFACE SOKA AND OTHERS**
**DEFENDANT/RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE OF MENTION /HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for Mention/hearing on **29 day of 05, 2023 at 9:00 am.** Before Hon **REHEMA LYANA SRM/RM**

**YOUR ARE** required to appear in this court without fail and you must produce to that day all the document upon which you intend to reply in support of your case.

Given under my hand and seal of the Court this **18 day of 5,2023**

SENIOR/ RESIDENT MAGISTRATE

DISTRICT COURT ILALA P. O. Box 270

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ISAYA AGUSTINO MDINGIU** anatangaza kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI yenye namba za usajili **MC 194 CRG. YENYE CHASES NAMBA: LC6PCJK23L0038719. ENGINE NO; 156FM15AD2F77908**. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/166147/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROBERT WILLIAM MAEDA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 765 DHK – TOYOTA VITZ. Chassis no KSP902005582. ENGINE NO 1KR0330228.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/17508/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VITUS KANISIUS KAPINGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA PIAGGIO YENYE NAMBA ZA USAJILI T.683 CED.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/143768/2023**

## HARVESTER CAPITAL INVESTMENT LTD NOTISI/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**HARVESTER CAPITAL INVESTMENT** kwa idhini tuliyopewa na **SME IMPACT FUND TANZANIA LIMITED** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama zilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi/ Tangazo hili endapo hatalipa deni lake.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | AMOWA ENTERPRISES COMPANY LIMITED | ABTAHIYU RAMADHAN MWAHU | **A. GODOWN** LILILOPO MKOA WA NJOMBE MAKAMBAKO **PLOT NO. 35 BLOCK A MTEWELE VILLAGE**<br>**B. NYUMBA** ILIYOPO MKOA WA NJOMBE,<br>**PLOT NO. 118 BLOCK G MAKAMBAKO AREA** | 07.06.2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | SAMWEL DAUDI SHILYA | - | **NYUMBA NA GODOWN/ (GHALA)** ZILIZOPO MKOA WA GEITA WILAYA YA BUKOMBE KITONGOJI CHA MWALU | 17.06.2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/ dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindi wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/ eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**
**HARVESTER CAPITAL INVESTMENT**
**P.o.Box 11898**
**ARUSHA**
**Tel: 0784 200283/ 0767 529 605**
**Email: harvestercapital558@gmail.com**

## KUPOTEA KWA CHETI



**TWAHA HAMIS SHABAN** anatangaza kupotelewa na Certificate NTA Level 5 chenye namba **NS1334/0090/2015** kilichotolewa na **ARDHI INSTITUTE TABORA** mwaka 2019. Diploma NTA Level 6 chenye namba **NS1334/0090/2015** kilichotolewa na **ARDHI INSTITUTE TABORA** mwaka **2020.**
Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **DAR/CHU/RB/174801/2023 / DAR/CHU/RB/35494/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**TWAHA HAMIS SHABAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1334-0090** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MHONGOLO PROGRESSIVE SEKONDARI** mwaka 2015. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0314-0679 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KAZIMA SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **DAR/CHU/RB/35490/2023 / DAR/CHU/RB/35493/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO W A TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MOROGORO**
**SHAURI LA MAOMBIU MADOGO YA MADAI NA. 22 YA 2022**

**ANTHONY CHIKOTI......................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**WILLIUM BEATUS LIMBE ................. MJIBU MAOMBI**

**WITO WA MAHAKAMANI**

**KWA: WILLIUM BEATUS LIMBE**
Wito huu ni wa kesi tajwa hapo juu, ambayo imepangwa kutajwa tarehe 29 mwezi wa 5 mwaka 2023 saa 03:00 asubuhi mbele ya Mheshimiwa **Jaji M.J. CHABA.**
Unatajkwia kuhudhuria wewe binafsi au wakili uliyemuidhinisha kusimama kwa niaba yako na pia unatakwia kutoa maelezo yako siku hiyo na nakala zote za ushahidi utakazo tumia kwa shauri hili .
Zingatia kwamba , kutohudhuria siku ya kesi na kwa wakati uliotajwa hapo juu, Mahakama itaendelea kusikiliza shauri hili na kutoa maamuzi bila ya uwepo wako.
Imetolewa chini ya Muhuri wa Mahakama Kuu Kanda ya Morogoro leo siku ya tarehe **2 mwezi wa o05 Mwaka 2023 .**

NAIBU MSAJILI MAHAKAMA KUU
MOROGORO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAINLINE CARRIERS LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 551 BKC.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **DAR/MBA/RB/174399/2023.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Kilolo......KILOLO**
**Kituo cha KILOLO.............MKOA ............IRINGA**
**Shauri la madai/Ndoa No 05/2023**
**Jina la mdai ANTONY EXPEDITO LWIMBO**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa HARUNA MUHANGA**
**UNAAMULIWA NA MAHAKAMA KUJA KUJIBU KESI YA MADAI NO 05/2023 DHIDI YA ANTONY EXPEDITO LWIMBO.**
Kwahiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 01 mwezi 06 mwaka 2023 saa 8:30 asubuhi bila kukosa. Kwa mujibu wa madai hayo na kwakuwa siku hiyo nisiku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi /mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO**; Kama hautohudhuria siku hiyo na ikathibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yawewe kuwepo
Hati hii imetolewa leo tarehe 15 mwezi wa 05 mwaka 2023

HAKIMU

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Maradhi uti wa mgongo yaua watu 102 Niger

**ZINDER, Niger**

WIZARA ya Afya ya Niger imesema imeshirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuzindua kampeni ya chanjo dhidi ya homa ya uti wa mgongo ambayo imeua watu 102 tangu mwezi Januari, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la AFP, visa hivyo vimetokea hasa katika eneo la Zinder kusini mwa Niger, huku wizara ikibainisha kuwa wengi waliofariki ni watoto na kwamba zaidi ya wagonjwa 1,810 walirekodiwa.

Wizara ilibainisha kuwa eneo hilo la Zinder, linalopakana na Nigeria, ndilo lililoathiriwa zaidi likiwa na wagonjwa zaidi ya 1,470 na vifo 84.

Kwa mujibu wa televisheni ya taifa hilo, Niger na WHO wamezindua kampeni ya chanjo katika mji wa Zinder inayolenga takriban watu 380,000 kuanzia Mei 17 hadi 25 mwaka huu.

WHO ilieleza kuwa eneo la Zinder linapakana na jimbo la Jigawa la nchini Nigeria, ambako ugojwa huo pia uliripotiwa, ikitahadharisha kwamba kuna hatari ya ugonjwa huo kusambaa katika maeneo mengine ya jirani.

"Jambo jingine, kuonekana kwa wakati mmoja kwa magonjwa mengine ya milipuko, ukosefu wa usalama na kuhamishwa kwa raia, yote katika muktadha wa mzozo wa muda mrefu wa kibinadamu, kunaweza kuchangia kuenea kwa mlipuko katika nchi zingine za ukanda mdogo wa Afrika Magharibi," ilisema WHO.

WHO inatathmini hatari inayoletwa na mlipuko wa sasa wa homa ya uti wa mgongo nchini Niger kuwa ya juu katika ngazi ya kitaifa, ya wastani katika ngazi ya kanda na ya chini katika ngazi ya kimataifa.

Inaelezwa kuwa Niger mara kwa mara hukumbwa na milipuko ya ugonjwa wa uti wa mgongo kutokana na nafasi yake ndani ya ukanda wa uti wa mgongo barani afrika unaoenea katika bara zima, kutoka Senegal magharibi hadi Ethiopia mashariki.

Aidha, kwa mujibu wa takwimu za WHO nchini Niger, ugonjwa huo uliua takribani watu 200 mwaka 2017, hasa watoto, na kwamba mwaka 2015 homa hiyo iliua watu 577 kati ya wagonjwa zaidi ya 8,589 waliorekodiwa.

***RFI***



Kiwanda cha kusafisha mafuta cha tajiri mkubwa barani Afrika, Aliko Dangote kilichozinduliwa juzi na Rais wa Nigeria Muhammadu Buhari, ambacho kina uwezo wa kusafisha mapipa 650,000 kwa siku, huku kikitarajiwa kuanza kazi Juni mwaka huu. **PICHA: AFP**

## India yapitisha ulazima upimaji dawa ya kikohozi

**NEW DELHI, India**

SERIKALI ya India imewaamuru watengenezaji wa dawa za kikohozi kupima sampuli za dawa hizo kabla ya kuziuza nje ya nchi hiyo, ili kuepusha malalamiko juu ya madhara yanayodaiwa kusababishwa na baadhi ya dawa za kikohozi za zinazotoka nchini humo.

Inaelezwa kuwa kuanzia Juni mosi, mwaka huu, kampuni hizo zitalazimika kupata cheti cha uchambuzi kutoka kwa maabara iliyoidhinishwa na serikali.

Mabadiliko hayo ya sheria yanakuja baada ya baadhi ya dawa za kikohozi zilizotengenezwa India kuhusishwa na vifo nchini Gambia na Uzbekistan.

Mabishano hayo yalikuwa yameleta dosari katika tasnia ya dawa ya India ambayo inatoa theluthi moja ya dawa zinazotumika duniani.

Inaelezwa kuwa tangazo hilo lilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Biashara ya Kigeni, ambaye katika taarifa yake alisema kwamba dawa za kikohozi zitaruhusiwa kusafirishwa nje ya nchi baada ya sampuli ya dawa zitakazosafirishwa nje kuchunguzwa.

Pia ilitaja orodha ya maabara kuu na za serikali kote nchini ambazo zitahusika katika upimaji wa sampuli za dawa hizo.

Wiki iliyopita, Reuters iliripoti kwamba India ilikuwa ikizingatia mabadiliko ya sera baada ya dawa za kikohozi za taifa hilo kuhusishwa na vifo vya watoto baada ya kutumia katika mataifa mengine.

Kampuni nyingi za maduka ya dawa za India zimechunguzwa kwa ubora wa dawa zao, huku wataalamu wakiibua wasiwasi juu ya mazoea yao ya utengenezaji.

Mwezi Machi, mamlaka ya kudhibiti utengenezaji wa dawa nchini India alibatilisha leseni ya kampuni ya Marion Biotech, ambayo dawa zake za kikohozi zilihusishwa na vifo vya watoto 18 nchini Uzbekistan.

***BBC***

# Sitisho la mapigano laleta matumaini Sudan

**KHARTOUM, Sudan**

WANANCHI wa Sudan sasa wana matumaini kuwa kusitishwa mapigano kwa wiki moja kupisha juhudi za kibinadamu kutamaliza madhila wanayopitia, baada ya mfululizo wa matamko ya awali ya makabaliano kukiukwa.

Maofisa wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini Sudan walisema mapigano hayo yanaweza kugeuka kuwa mzozo wa kikabila endapo pande zinazozozana hazitaheshimu usitishaji mapigano ulioongezwa.

Mwakilishi maalum wa UN, nchini Sudan, Volker Perthes, ameliambia baraza la usalama la umoja huo kwamba kuongezeka kwa ukabila kunahatarisha kuongeza athari kwa eneo hilo.

Perthes alisema mwezi uliopita wa mapigano kulitokea dalili za kutishia kugawanya nchi hiyo kwa misingi ya kikabila na kijamii.

"Dalili za tahadhari za uhamasishaji wa kikabila pia zinaripotiwa katika maeneo mengine ya nchi, haswa katika mikoa ya Kordofan Kusini na Blue Nile.

"Mapigano nchini kote yamesababisha ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, sheria za kimataifa za kibinadamu na kudhoofisha ulinzi wa raia," alisema Perthes.

Aidha, baada ya kuanzisha usitishaji wa mapigano, aliliambia baraza la usalama, kipaumbele namba mbili cha UN ni kuzuia kuongezeka au kueneza ukabila katika mzozo huo.

Licha ya makubaliano yaliyovunjwa awali, raia waliochoshwa na vita wamebaki na matumaini kwamba usitishaji mapigano utaendelea ili kuruhusu usambazwaji wa misaada kama chakula, dawa na rasilimali nyingine muhimu.

Mmoja wa wananchi wa Sudan Adam Othman alisema "Makubaliano hayo ni mafanikio ya kweli kwa watu wa Sudan, yatapunguza mateso tunayopitia, suluhu ya vita duniani kote huanza na mazungumzo na mapatano, kwa hiyo tunatumaini kwamba mapatano haya yatakuwa na nafasi na yatatekelezwa ipasavyo."

Naye mkazi wa mji wa Nile Souad al-Fateh alisema "Tunataka makubaliano, walio madarakani wakubaliane, sote tuna njaa, watoto na wazee, kila mtu anateseka na vita, hatuna maji tena, tuna njaa kweli kweli, lazima wafikie makubaliano."

UN ilibainisha kuwa kwa sasa, nchini Sudani watu milioni 25 zaidi ya nusu ya watu wote wanahitaji misaada ya kibinadamu.

Aidha, kiongozi wa kundi la wapiganaji wenye nguvu nchini Sudan la (RSF), Mohamed Dagalo, alisema wapiganaji wake watatekeleza mkataba wa usitishaji mapigano ulioanza kutekelezwa juzi baada ya kutiwa saini mwishoni mwa juma lililopita nchini Saudi Arabia.

***VOA***

# WAZIRI CHANA APONGEZA JITIHADA EXIM KUINUA GOFU WANAWAKE

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Dk. Pindi Chana amepongeza jitihada za Benki ya Exim Tanzania katika kudhamini matukio mbalimbali ya wanawake nchini ikiwemo michezo huku akibainisha nia ya Serikali ya kushirikiana na wadau mbalimbali nchini ili kuboresha hali ya michezo nchini ukiwemo mchezo wa gofu.

Dk. Chana ameibainisha nia hiyo ya serikali wakati akiongoza hafla fupi ya kuhitimisha mashindano ya wazi ya mchezo wa gofu ya wanawake ya 'Lugalo Ladies Open 2023' yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa Klabu ya mchezo huo ya Lugalo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Mashindano hayo yaliratibiwa na Chama cha Golf cha Wanawake Tanzania (TLGU) na kufanyika kwenye viwanja vya Lugalo.

"Pamoja na kuipongeza Benki ya Exim Tanzania na wadau wengine waliojitokeza kufanikisha mashindano haya nitumie fursa hii kuwapa taarifa njema kwamba tayari Serikali imeanza kutekeleza jitihada kadhaa ili kuinua hali ya mchezo wa gofu nchini ikiwemo kukutana na wadau wa mchezo husika ili kujadili namna sahihi ya kuboresha mchezo huu pendwa," alisema Dk Chana.

Aidha, alisema Serikali inaangalia namna ya kuajiri mkufunzi wa kimataifa wa gofu nchini kufuatia ombi la wadau wa mchezo huo huku pia ikihakikisha nguvu zinazoelekezwa kwenye maboresho ya mchezo wa mpira wa miguu nchini zikielekezwa pia kwenye michezo mingine ukiwemo mchezo huo wa gofu.

Hafla hiyo iliyohudhuriwa na wacheza gofu wa kike kutoka vilabu mbalimbali nchini, ilikua fursa kwa benki ya Exim Tanzania kutangaza bidhaa yake mpya ya Supa Woman inayolenga kusaidia wanawake kusimamia fedha zao kwa ufanisi na kufikia malengo yao ya binafsi na kitaaluma.

Kwa upande wake, Mkuu wa bidhaa za rejareja na uhakika wa mapato wa benki hiyo, Mtenya Cheya, alisema kupitia bidhaa ya Supa Woman benki hiyo inajivunia kuunga mkono wanamichezo wa kike na kutambua mafanikio yao bora katika michezo .

" Tunatumai kuwa ushiriki wetu kwenye mashindano haya ya gofu utawatia moyo wanawake zaidi ili kufuata matamanio yao na kufikia malengo yao, ndani na nje ya uwanja wa gofu." alisema Mtenya.

Aidha Mwenyekiti wa Chama cha Gofu cha Wanawake nchini (TLGU) Queen Siraki alisema pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali kuendeleza michezo nchini pia alimuomba Waziri Chana kuwashawishi viongozi wakiwemo wabunge wanawake kushiriki kwenye mchezo huo ili kuongeza hamasa miongoni mwa wanawake nchini.




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Dk. Pindi Chana (wa tatu kulia) akikabidhi cheti cha utambuzi wa ushiriki kwa Mkuu wa Matawi wa Kanda Benki ya Exim Elizabeth Mayengoh (wa tatu kushoto) ikiwa ni ishara ya kutambua mchango mkuu wa benki hiyo katika kufanikisha mashindano ya wazi ya gofu ya Wanawake 'Lugalo Ladies Open 2023' wakati wa hafla fupi iliyofanyika mwishoni mwa wiki kwenye Ukumbi wa Klabu ya mchezo huo ya Lugalo jijini Dar es Salaam. Wengine ni Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Brigedia Jenerali Mstaafu Michael Luwongo (wa pili kulia), Rais wa Chama cha Mchezo huo cha Wanawake Tanzania (TLGU) Queen Siraki na wadau wengine wa mchezo huo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

# Azam FC 'yaipotezea' Yanga

**Na Hadija Mngwai**

AZAM FC imesema kwa sasa hawaifikirii fainali ya kombe la Shirikisho (FA) badala yake akili zao zipo kwenye michezo yao miwili ya mwisho ya ligi kuu Tanzania Bara ambapo wanataka kumaliza vizuri mechi hizo za mwisho msimu huu.

Azam FC imetinga Fainali ya FA ikitarajia kucheza na Yanga kwenye Uwanja wa Mkwakwani mkoani Tanga, na kwenye ligi inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 53 ikipishana kwa pointi mbili dhidi ya Singida Big Stars yenye pointi 51 wakivutana kumaliza katika nafasi hiyo.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Habari wa Azam FC, Thabiti Zakaria 'Zaka' amesema kuwa wanachokiangalia hivi sasa ni mechi zao mbili za ligi kuhakikisha wanaibuka na pointi sita zilizobakia kwa kuwa fainali ya FA bado haijapangwa.

"Hii mechi ya FA bado hatujui itachezwa lini kwa sababu TFF bado hawajaipangia ratiba, hatuwezi kuifikiria kwa sasa, sisi tunaelekeza nguvu kwenye michezo yetu miwili ya mwisho kwenye ligi na baada ya hapo ndipo tutaanza mikakati kwa mchezo huo wa fainali baada ya kufahamu tarehe ya mchezo," alisema Zaka.

Alisema kujiandaa na michezo hiyo miwili ya mwisho, awali waliweka kambi lakini baada ya bodi ya ligi kupangua ratiba waliamua kuvunja kambi na kuwapa wachezaji wao mapumziko mafupi.

"Lakini kwa sasa wachezaji wamerejea kwenye mazoezi kujiandaa na michezo hii miwili, malengo yetu ni kuhakikisha tunamaliza vizuri ligi msimu huu kwa kusanya pointi zote sita zilizosalia," alisema Zaka.

Bodi ya ligi imetangaza michezo ya mwisho kuhitimisha msimu huu wa ligi kuu itachezwa Juni 9.

## NBC yazindua Dodoma Marathon 2023

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NBC jana imezindua rasmi msimu wa nne wa mbio za marathoni za 'NBC Dodoma Marathon 2023' zilizopangwa kufanyika Julai 23 mkoani humo.

Mbio hizo zina lengo la kukusanya fedha ili kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi na kutoa ufadhili wa elimu kwa wanafunzi wanaosomea taaluma ya ukunga ili kuboresha afya ya mama wa mtoto.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya uzinduzi wa usajili wa mbio hizo iliyofanyika jijini Dar es Salaam mapema hii leo, Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya NBC Waziri Barnabas alisema pamoja na lengo la kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi lakini wameona umuhimu wa kuweka lengo lingine la kutoa ufadhili wa elimu kwa wanafunzi wanaosomea taaluma ya ukunga.

"Tukiwa tunazindua usajili wa mbio hizi leo (jana) habari njema ni kwamba NBC Dodoma Marathon imeongeza ajenda ya pili muhimu tukiwa na lengo la kuongeza thamani ya mbio hizi, awali tulikuwa na agenda moja pekee ambayo ni kuchangia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake tukishirikiana na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), lakini kufuatia mafanikio tunayoendelea kuyapata tukaona ipo haja ya kuongeza agenda nyingine mpya ambayo ni kuchangia katika kuboresha afya ya uzazi kupitia ufadhili wa elimu kwa wanafunzi wanaosomea taaluma ya ukunga kwa tukishirikiana na mdau mpya ambae ni Taasisi ya Benjamin Mkapa," alisema Barnabas.

Kwa mujibu wa Barnabas kupitia ufadhili wa wanafunzi wa elimu ya ukunga mbio hizo zitasaidia kukabiliana na upungufu wa wataalamu hao na hivyo kupunguza vifo vya kina mama wakati wa uzazi.

Alisema mpaka sasa tangua kuanzishwa kwa mbio hizo wameshakusanya zaidi ya shilingi milioni 500 zilizosaidia kufikia upimaji wa saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake zaidi ya 23,500 na matibabu kwa zaidi ya wanawake 1,300.

Aidha Bw Barnabas aliwashukuru wadau wa mashirika na makampuni mbali mbali kama Sanlam, Jubilee General Insurance, Garda World, Cheknocrafts, Icea Lions Insurance, Metropolitan Life Insurance, Strategies Insurance, Hans Paul, SBC- Pepsi, na Aramex kwa udhamini wao ili kufanikisha mbio hizo.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**BAYERN YAJITOSA KWA RICE**
KLABU ya Bayern Munich inamwona Declan Rice kama kiungo bora zaidi kwao, lakini inafahamu fika kuwa Arsenal pia inapania kumsajili mchezaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 24. ***(Sky Sport Germany)***

**NEYMAR AWANIWA MAN**
MANCHESTER United ipo kwenye mazungumzo juu ya mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 31 kutoka Paris St-Germain. ***(L'Equipe)***

**KIM NAE AWINDWA**
MANCHESTER United pia wanajaribu kukamilisha dili la kumnunua mchezaji wa Napoli, Kim Min-jae mwenye umri wa miaka 26, huku PSG wakimtaka beki huyo wa Korea Kusini. ***(Sun)***

**NEVES ATAKIWA BARCA**
BARCELONA wanataka kumsajili kiungo wa kati wa Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 26 kutoka Wolves msimu huu wa majira ya joto, lakini hatua hiyo itategemea ikiwa mshambuliaji wa Hispania, Ansu Fati mwenye miaka 20 kama ataondoka Barca. ***(The Athletic)***

**WATAFUTA MBADALA**
IKIWA Arsenal haitafanikiwa kumsajili Declan Rice, wamepanga kumchukua kiungo wa kati wa Real Sociedad na Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 24, na kiungo wa kati wa Brighton wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye miaka 21 kama mbadala. ***(Mail)***

**XHAKA HAKIJAELEWEKA**
KIUNGO wa kati wa Uswisi, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 30 amesema mustakabali wake utaamuliwa kabla ya mechi ya mwisho ya Arsenal msimu huu, huku kukiwa na ripoti kwamba yupo katika mazungumzo na Bayer Leverkusen kuhusu uhamisho wa pauni milioni 13. ***(Standard)***

**BALOGUN AWANIWA MILAN**
AC Milan imefanya Folarin Balogun wa Arsenal kuwa mlengwa wao mkuu wa uhamisho baada ya mshambuliaji huyo wa Marekani mwenye umri wa miaka 21, kuonesha kiwango cha juu wakati alipokuwa Reims kwa mkopo msimu huu, lakini watakabiliwa na ushindani kutoka kwa RB Leipzig. ***(Calciomercato)***

**VINICIUS HANA MPANGO**
MCHEZAJI Vinicius Junior hana mpango wa kuondoka Real Madrid, licha ya winga huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 22 kukumbwa na ubaguzi wa rangi kutoka kwa mashabiki. ***(90 Min)***

**GUEHI AGOMBEWA**
LIVERPOOL imejiunga na orodha ndefu ya klabu zinazotaka kumsajili beki wa England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 22 kutoka Crystal Palace. ***(Mail)***

**MACALLISTER NA LIVER**
LIVERPOOL inakaribia kuafikiana na kiungo wa kati wa Brighton mwenye umri wa miaka 24 na Argentina. Alexis Mac Allister. ***(Fabrizio Romano)***

**MARTIAL KUACHIWA**
KLABU ya Manchester United iko tayari kumwacha Anthony Martial aondoke baada ya kushindwa kumvumilia mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 27. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI ASUBIRIWA KUAMUA MWENYEWE KUTUA BARCA

●●●Kocha Xavi asema kujiunga tena na mabingwa hao wa Hispania inategemea nia ya nyota huyo....

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez amesema uwezekano wa Lionel Messi kurejea katika klabu hiyo ya Katalunya msimu ujao inategemea sana nia ya mshambuliaji huyo wa Argentina.

Messi anamaliza mkataba na klabu ya Paris Saint-Germain mwishoni mwa msimu huu, huku vyanzo vya habari vikiiambia ESPN kwamba ataachana na klabu hiyo ya Ufaransa. Messi anavutiwa na klabu za Saudi Arabia na Marekani, lakini Barca wana matumaini ya kumrejesha licha ya matatizo ya muda mrefu ya kifedha ambayo yalisababisha kuondoka kwake mwaka 2021.

"Ni suala la hali itakuwaje," alisema Xavi katika mkutano na waandishi wa habari jana alipoulizwa kuhusu nafasi ya Barca kumsajili Messi.

"Inategemea mambo mengi. Sina mengi zaidi ninaweza kusema, Messi ni mwanasoka wa kuvutia. Ni rafiki. Kutoka hapo, inategemea mambo mengi, lakini juu ya yote nia yake na kile anachotaka."

Messi, ambaye anatimiza umri wa miaka 36 Juni, anaweza kulipwa kiasi kikubwa zaidi nchini Saudi Arabia, lakini haiba ya Barca kumrejesha imeongezeka katika wiki za hivi karibuni, huku makamu wa rais Rafa Yuste pia akieleza nia yake ya kutaka kumsajili.

"Nataka arudi, huo ndio ukweli," alisema Yuste akiiambia DAZN Jumamosi baada ya Barca kukabidhiwa kombe la Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, kwenye uwanja wa Spotify Camp Nou.

"Baada ya kila kitu alichoipa klabu hii, akipitia akademi, akianzia kucheza hapa... ni hadithi nzuri na hadithi nzuri lazima ziwe na mwisho wa furaha.

"Ikiwa kila kitu kitaenda sawa na hata kama atalazimika kufanya uamuzi wa mwisho natumaini atarejea. Sote tutafurahi sana," alisema Xavi.

Barca wamewasilisha mpango wa kutekelezwa kwa LaLiga wakieleza kasoro watakazofanya katika kipindi cha miaka miwili ijayo ili kusajili mikataba mipya inayotolewa kwa wachezaji wa sasa wa kikosi cha kwanza, akiwamo Ronald Araujo na Gavi, pamoja na kufanya usajili msimu huu wa majira ya joto.

Barca wamekosa beki wa kulia katika kipindi cha pili cha msimu, lakini Xavi alisema kipaumbele ni kutafuta mbadala wa Sergio Busquets, ambaye ameamua kutoongeza mkataba wake na klabu hiyo.

"Beki wa kulia sio kipaumbele nambari moja," alisema bosi huyo wa Barca.

"Busquets anakwenda kwa hivyo ni dhahiri tunahitaji kiungo wa ulinzi wa kiwango cha juu kwa msimu ujao.

"Nahodha wetu anaondoka, hivyo tunahitaji mchezaji mzuri sana ili aingie, tunapaswa kuchukua nafasi yake kwa njia bora zaidi, kutoka hapo, kuna vipaumbele vingine na tunapoimarisha zaidi, tunataka kuwa na ushindani zaidi."

ESPN iliripoti Machi kwamba, Inigo Martinez, Ilkay Gundogan na Ruben Neves ni miongoni mwa wachezaji wengine wanaotarajiwa kusajiliwa msimu huu wa majira ya joto pale Barca.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,117,4

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 24 NA 25 MEI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 24/05/23 | 20:00 | Djurgardens IF vs BK Hacken | 2.30 | 3.39 | 2.62 |
| 02. 24/05/23 | 21:45 | Ross County vs St Johnstone | 2.37 | 3.15 | 2.89 |
| 03. 24/05/23 | 21:45 | Livingston vs Motherwell | 2.89 | 3.10 | 2.40 |
| 04. 24/05/23 | 21:45 | Dundee Utd vs Kilmarnock | 2.38 | 3.20 | 2.83 |
| 05. 24/05/23 | 23:00 | Espanyol vs Atletico Madrid | 2.75 | 3.35 | 2.33 |
| 06. 25/05/23 | 01:00 | Patronato Parana vs Olimpia Asuncion | 2.47 | 3.12 | 2.67 |
| 07. 25/05/23 | 01:00 | Juventude RS vs Atletico GO | 2.36 | 3.17 | 2.77 |
| 08. 25/05/23 | 01:00 | Londrina PR vs Ceara CE | 2.70 | 3.05 | 2.50 |
| 09. 25/05/23 | 03:30 | Criciuma SC vs Sport Recife | 2.34 | 3.02 | 2.92 |
| 10. 25/05/23 | 05:00 | FBC Melgar vs Atletico Nacional | 2.32 | 3.17 | 2.83 |
| 11. 25/05/23 | 20:30 | Mallorca vs Valencia | 3.40 | 2.95 | 2.19 |
| 12. 25/05/23 | 20:30 | Ankaragucu vs Basaksehir | 2.64 | 3.31 | 2.39 |
| 13. 25/05/23 | 21:30 | Grasshoppers vs St. Gallen | 2.49 | 3.57 | 2.49 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# XHAKA: ARTETA NI ZAIDI YA KOCHA ARSENAL

**LONDON, England**

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Granit Xhaka anaamini kwamba, Mikel Arteta ndiye mtu sahihi wa kuipeleka mbele klabu hiyo.

Matumaini ya Washikabunduki hao kutwaa taji la Ligi Kuu ya England yalimalizika Jumamosi walipopoteza 1-0 dhidi ya Nottingham Forest, ambao walishuhudia Manchester City wakitawazwa mabingwa kwa mara ya tano ndani ya misimu sita.

Lakini walikaa kileleni mwa ligi kwa siku 248 za msimu na walikuwa na uongozi wa pointi nane dhidi ya City Machi, lakini licha ya kuchelewa kwao kushika nafasi ya kwanza kikosi cha Arteta kimepata sifa kwa maendeleo yao msimu huu.

Alipoulizwa kama alidhani Arteta ndiye angeweza kuwaongoza katika harakati za kuwakimbiza City, alisema: "Unaweza kusahau swali hilo - yeye ni zaidi ya kocha sahihi wa timu hii."

Arsenal wamepoteza vibaya katika mechi zao nane zilizopita, wakishinda mara mbili pekee, lakini Xhaka amesema msimu huu unapaswa kuwa msingi wa kusonga mbele.

"Hatuhitaji kusahau jinsi tulivyofanya kazi kwa miezi 11 iliyopita," alisema.

"Hata tulipopoteza katika michezo miwili iliyopita, bila shaka watu wanaona kinachotokea sasa, lakini usisahau miezi 11 tuliyofanya kazi.

"Ikiwa mtu alituambia kabla ya msimu kuwa tutakuwa hapa, nadhani kila mtu asingeamini. Lengo letu la uhakika lilikuwa kurejea katika nafasi nne za juu. Sasa sisi ni wa pili. Bila shaka unapokuwa karibu sana na taji unataka kushinda taji.

"Lakini tupo pale tulipo, tunastahili kuwa hapa tulipo, na tuone nini kitatokea msimu ujao. Tunapaswa kwenda na kufanya hatua inayofuata."

# MacAllister njia nyeupe Liverpool

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Liverpool na kiungo wa kimataifa wa Argentina anayekipiga klabu ya Brighton kila kitu kipo sawa na sasa ni suala kwa mchezaji huyo kutua Anfield.

Liverpool imeshafikia makubaliano ya kumsajili mchezaji huyo ambaye yeye mwenyewe ameonesha nia ya kujiunga na klabu hiyo.

Hadi sasa majogoo wa Anfield wameshakubaliana maslahi binafsi na MacAllister kilichobakia ni kulipa ada ya uhamisho kwa Brighton.

Dalili za kiungo MacAllister kuondoka ndani ya Brighton zilionekana pale ambapo kocha wa klabu hiyo, Roberto de Zerbi aliposema kuwa inawezekana akawakosa wachezaji wake muhimu ndani ya msimu ujao.

Huku majina kama MacAllister na Moises Caicedo yakiwa yametajwa kuwa wanaachana na klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu.

Liverpool inaelezwa inataka kuharakisha zaidi nafasi ya kiungo na walikuwa wa kwanza kumwania MacAllister ambaye alikuwa akiwindwa na Manchester United.

MacAllister amekuwa na msimu bora ndani ya Brighton pamoja na timu ya taifa ya Argentina ambapo alikuwa moja ya wachezaji muhimu walioisaidia timu hiyo kutwaa ubingwa wa dunia.



## HABARI MICHEZO


17,539/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/05/23 | 19:00 | ACF Fiorentina vs AS Roma | 2.40 | 3.20 | 2.75 |
| 02. 27/05/23 | 20:00 | Sevilla FC vs Real Madrid | 2.80 | 3.40 | 2.29 |
| 03. 27/05/23 | 22:00 | Montpellier HSC vs OGC Nice | 2.47 | 3.30 | 2.60 |
| 04. 28/05/23 | 02:30 | Orlando City SC vs Atlanta United FC | 2.15 | 3.10 | 2.85 |
| 05. 28/05/23 | 15:30 | Carlisle United vs Stockport County FC | 3.00 | 3.15 | 2.28 |
| 06. 28/05/23 | 15:30 | AZ Alkmaar vs PSV Eindhoven | 2.55 | 3.50 | 2.40 |
| 07. 28/05/23 | 15:30 | Fortuna Sittard vs NEC Nijmegen | 2.50 | 3.40 | 2.50 |
| 08. 28/05/23 | 16:00 | AC Monza vs US Lecce | 2.70 | 3.10 | 2.50 |
| 09. 28/05/23 | 17:15 | Racing Santander vs FC Cartagena | 2.55 | 3.05 | 2.65 |
| 10. 28/05/23 | 18:30 | Chelsea FC vs Newcastle United | 2.80 | 3.35 | 2.29 |
| 11. 28/05/23 | 18:30 | Aston Villa vs Brighton & Hove Albion | 2.16 | 3.55 | 2.90 |
| 12. 28/05/23 | 18:30 | Leeds United vs Tottenham Hotspur | 2.65 | 3.45 | 2.34 |
| 13. 28/05/23 | 20:00 | Cadiz CF vs RC Celta de Vigo | 2.65 | 3.15 | 2.50 |
| 14. 28/05/23 | 20:00 | Getafe CF vs CA Osasuna | 2.50 | 3.15 | 2.70 |
| 15. 28/05/23 | 20:00 | Girona FC vs Real Betis Seville | 2.60 | 3.15 | 2.60 |
| 16. 28/05/23 | 21:45 | Juventus Turin vs AC Milan | 2.26 | 3.25 | 2.95 |
| 17. 28/05/23 | 22:00 | SC Corinthians SP vs Fluminense FC RJ | 2.70 | 3.05 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 24/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1895 | Kolos Kovalivka vs Dynamo Kiev | 5.96 | 3.90 | 1.46 |
| 13:00 | 2120 | Yokohama vs Sanfrecce Hiroshima | 5.78 | 4.44 | 1.42 |
| 13:00 | 2186 | Seongnam Ilhwa vs Pohang Steelers | 3.94 | 3.47 | 1.79 |
| 13:00 | 2520 | Kashima Antlers vs Kashiwa Reysol | 1.83 | 3.42 | 3.84 |
| 13:00 | 3562 | Niigata Albirex vs Avispa Fukuoka | 2.37 | 3.06 | 2.85 |
| 13:00 | 3583 | FC Tokyo vs Cerezo Osaka | 2.32 | 3.21 | 2.80 |
| 13:00 | 3861 | Incheon Utd vs Gyeongnam | 1.79 | 3.53 | 3.89 |
| 13:00 | 4678 | Gamba Osaka vs Kyoto Sanga | 1.70 | 3.68 | 4.15 |
| 13:00 | 4948 | Seoul E Land vs Gwangju | 3.23 | 3.23 | 2.08 |
| 13:00 | 5455 | Suwon Samsung vs Daegu | 2.54 | 3.12 | 2.60 |
| 13:00 | 5467 | Jeju Utd vs Daejeon Citizen | 2.09 | 3.27 | 3.17 |
| 13:00 | 5811 | Jeonbuk Hyundai vs Paju Citizen FC | 1.24 | 5.39 | 9.11 |
| 13:00 | 5936 | Jeonnam Dragons vs Ulsan Hyundai | 5.17 | 4.09 | 1.51 |
| 14:35 | 3690 | Shanghai SIPG vs Henan Jianye | 1.21 | 5.13 | 11.28 |
| 15:00 | 2330 | Veres Rivne vs Oleksandria | 2.77 | 3.29 | 2.25 |
| 16:00 | 2242 | Selangor FC vs Kedah | 1.56 | 4.13 | 4.43 |
| 16:00 | 5736 | Kuala Lumpur vs Kuching FA | 1.23 | 5.33 | 9.22 |
| 17:00 | 5517 | Zorya Lugansk vs Shakhtar Donetsk | 3.70 | 3.55 | 1.79 |
| 18:00 | 1584 | Nomme Kalju vs Tammeka Tartu | 1.73 | 3.51 | 4.24 |
| 18:00 | 1710 | Varnsdorf vs MFK Karvina | 2.44 | 3.14 | 2.62 |
| 18:00 | 2904 | Fotbal Trinec vs Opava | 2.48 | 3.02 | 2.66 |
| 18:00 | 2974 | Blansko vs FC Slovan Rosice | 2.65 | 3.33 | 2.37 |
| 18:00 | 4252 | Dukla Prague vs SK Prostejov | 1.51 | 4.01 | 5.04 |
| 18:00 | 4284 | SFK Vrchovina vs Hlucin | 5.79 | 4.24 | 1.45 |
| 18:00 | 5085 | Vyskov vs Jihlava | 1.52 | 4.06 | 4.83 |
| 18:00 | 5498 | KS Warta Sieradz vs Olimpia Zambrow | 2.07 | 3.53 | 3.01 |
| 19:00 | 2870 | AEL Limassol vs Omonia Nicosia | 3.11 | 2.85 | 2.33 |
| 20:00 | 1071 | Pardubice vs Baumit Jablonec | 2.06 | 3.48 | 3.27 |
| 20:00 | 1258 | Hajduk Split vs HNK Sibenik | 1.39 | 4.46 | 6.43 |
| 20:00 | 1995 | Teplice vs Zbrojovka Brno | 2.42 | 3.48 | 2.64 |
| 20:00 | 3246 | Djurgardens IF vs BK Hacken | 2.34 | 3.33 | 2.62 |
| 20:00 | 5004 | Zlin vs Banik Ostrava | 2.29 | 3.36 | 2.89 |
| 20:30 | 1694 | Real Madrid vs Rayo Vallecano | 1.69 | 3.74 | 4.31 |
| 20:30 | 2514 | Fenerbahce vs Sivasspor | 1.49 | 4.03 | 5.58 |
| 20:30 | 2848 | Villarreal vs Cadiz CF | 1.45 | 4.38 | 5.77 |
| 20:30 | 3291 | AEK Athens vs PAOK | 2.01 | 3.15 | 3.52 |
| 20:30 | 3839 | Sepsi Osk vs Universitatea Cluj | 1.99 | 3.21 | 3.52 |
| 20:30 | 4814 | Elche vs Sevilla FC | 3.95 | 3.60 | 1.79 |
| 21:00 | 1401 | Senegal U20 vs Israel U20 | 1.95 | 3.17 | 3.68 |
| 21:00 | 3322 | Italy U20 vs Nigeria U20 | 1.95 | 3.21 | 3.63 |
| 21:45 | 2526 | Ross County vs St Johnstone | 2.20 | 3.20 | 3.14 |
| 21:45 | 3150 | Livingston vs Motherwell | 2.89 | 3.10 | 2.40 |
| 21:45 | 3859 | Rangers vs Hearts | 1.35 | 5.05 | 6.94 |
| 21:45 | 4398 | Dundee Utd vs Kilmarnock | 2.38 | 3.20 | 2.83 |
| 21:45 | 5844 | Hibernian vs Celtic | 5.86 | 4.61 | 1.43 |
| 21:45 | 5916 | Aberdeen vs St Mirren | 1.93 | 3.36 | 3.72 |
| 22:00 | 1997 | Fiorentina vs Inter | 3.66 | 3.34 | 1.99 |
| 22:00 | 5035 | Brighton vs Manchester City | 3.61 | 3.80 | 1.82 |
| 23:00 | 2334 | Betis vs Getafe | 1.99 | 3.11 | 3.76 |
| 23:00 | 3389 | Espanyol vs Atletico Madrid | 2.75 | 3.35 | 2.33 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MAYELE, AZIZ KI VINARA MABAO MGUU WA KULIA, KUSHOTO KWENYE LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mshambuliaji Fiston Mayele akiwa ameshaweka nyavuni mabao 16 na kuendelea kuongoza kwenye orodha ya wafungaji, nyota huyo ameweka rekodi nyingine ya kuongoza kwa kufunga mabao mengi kwa mguu wa kulia mpaka sasa.

Mayele amefunga jumla ya mabao 12 kwa kutumia mguu wa kulia tu, huku nafasi ya pili ikichukuliwa na mshambuliaji wa Prisons, Jeremiah Juma aliyepachika mabao manane, Pape Sakho wa Simba akiwa kwenye nafasi ya tatu kwa kupachika mabao manane, nafasi ya nne ikienda tena kwa mchezaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza akipachika mabao saba.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu Tanzania Bara, kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki amefunga jumla ya mabao tisa kwa mguu wa kushoto na kuwa kinara mpaka sasa kwa upachikaji mabao kutumia mguu huo hadi kufikia raundi ya 28.

Straika wa Simba Moses Phiri anashika nafasi ya pili akiwa amefunga mabao matano kwa kutumia mguu huo, mabao manne yalikuwa yamefungwa na Augustine Okra wa Simba akikamata nafasi ya tatu.

Jumla ya wachezaji watano wako kwenye nafasi ya nne wakiwa wamefunga mabao matatu kwa mguu wa kushoto,wacheaji hao ni Edwin Balua wa Prisons, Gustaph Saimon wa Coastal Union, Kassim Suleiman wa Ruvu Shooting, Nickson Kibabage wa Singida Big Stars na Shiza Kichuya wa Namungo.

Takwimu hizo zinaonyesha kuwa straika wa Polisi Tanzania, Kelvin Sabato anaongoza kwa kutupia mabao kwa vichwa, akiwa na mabao matano mpaka sasa.

Anafuatiwa na Rafael Daudi wa Ihefu mwenye mabao manne, huku wachezaji wa Simba raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Henock Inonga na Jean Baleke, wanashika nafasi ya tatu kwa kufunga mabao matatu kila mmoja.




Mratibu wa Kampuni ya 361 Degrees Africa, Benedict Msofe, akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu tuzo za harusi awamu ya tatu zinazotarajiwa kufanyika Mei 28 jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mshauri wa Biashara wa Kampuni ya Innovex Tanzania, Bahya Tajiri na Meneja wa Hoteli ya Regency, Lilian Maduda. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Nabi anasa

INATOKA UK. 24

tunamaliza kazi kwenye mchezo wetu wa nyumbani, tupate ushindi mzuri ambao utatupa picha ya nini cha kufanya kuelekea kwenye mchezo wa marudiano," alisema Nabi.

Yanga inahitaji ushindi mzuri kwenye mchezo wa kwanza hapa nyumbani kabla ya kuelekea jijini Alger nchini Algeria kwa ajili ya mchezo wa marudiano.

## Fedha za Super League

INATOKA UK. 24

wako kwenye mawindo makali na kama kocha wao Robertinho (Oliviera) atamtaka mchezaji huyo watakaa meza moja kumsajili.

"Sio Bajana tu, mchezaji yeyote ambaye kocha wetu atapendekeza tutakaa naye kwa ajili ya mazungumzo na kama ana mkataba na klabu nyingine basi tutakaa na klabu hiyo kuangalia namna ya kumsajili, Simba ni timu kubwa hivyo wachezaji wengi wanatamani siku moja kuichezea," alisema Ahmed.

Hata hivyo, Nipashe inafahamu Simba wameanza mazungumzo na Bajana kuangalia uwezekano wa kumsajili hasa baada ya nyota huyo kueleka ukingoni kumaliza mkataba wake na waajiri wake wa sasa, Azam FC.

Akizungumza na Nipashe jana, Bajana alikiri kufanya mazungumzo na uongozi wa Simba kwa ajili ya kumsajili.

"Sasa ni mapema kusema msimu ujao nitacheza wapi, kwa sababu mkataba wangu kwa sasa upo ukiongoni, nafanya mazungumzo na Azam FC kwa ajili ya mkataba mpya lakini Simba wameonyesha nia ya kunisajili, soka ni kazi yangu naangalia maslahi zaidi kwa sababu nina familia ambayo inanitegemea, je ni kubaki Azam FC au kwenda Simba ni suala la nani mwenye ofa nzuri," alisema Bajana.

# Michezo

Jumatano Mei 24, 2023
Nipashe



Messi asubiriwa kuamua mwenyewe kutua Barca UKURASA 21



# NABI ANASA FAILI LA WAARABU

## ●●●Asisitiza kumaliza kazi nyumbani kabla ya kuelekea Algeria kwenye mchezo wa...

Beki wa Yanga, Mamadou Doumbia (kushoto), akiondoa mpira mbele ya kiungo wa Singida Big Stars, Deus Kaseke, kwenye mchezo wa nusu fainali ya kombe la FA mwishoni mwa wiki iliyopita Uwanja wa Liti mkoani Singida, Yanga ilishinda bao 1-0 na kutinga hatua ya fainali ya michuano hiyo, sasa itakutana na Azam FC. **PICHA: SALEH JEMBE**

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Yanga, Nasreddine Nabi amesema amefahamu ubora na udhaifu wa wapinzani wao wa mchezo wa fainali ya kombe la Shirikisho Afrika USM Alger baada ya kunasa faili la Waarabu hao.

Nabi aliuagiza uongozi wa klabu hiyo kumtafutia mikanda ya video ya hivi karibuni ya wapinzani hao na tayari amekabidhiwa.

Yanga wataanzia nyumbani mchezo wa fainali Mei 28 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam kabla ya kurudiana nao Juni 3, mwaka huu nchini Algeria.

Akizungumza na Nipashe jana, Nabi alisema tayari kwa kupitia video alizopewa ameona ubora na udhaifu wa wapinzani wao hao na kwa sasa anafanyia kazi mbinu zitakazomwezesha kupata ushindi kwenye mchezo wa kwanza nyumbani.

Nabi alisema michezo hiyo miwili ya fainali ni michezo ya matokeo zaidi hivyo anaandaa mbinu itakayowapa matokeo mazuri kwenye michezo yote ili kuweza kutwaa ubingwa wa Afria kwa mara ya kwanza.

"Mechi itakuwa ya ushindani mkubwa nalihitaji kuwafuatilia wapinzani wetu jinsi wanavyocheza wanapokuwa ugenini na nyumbani, nafurahi nimepata mikanda yao na bado tunaendelea kuifanyia kazi ingawa nimeona ubora na hata udhaifu wa wapinzani wetu, mechi hizi mbili ni mechi za matokeo zaidi," alisema Nabi.

Alisema moja ya kazi aliyoifanya ni kuwabaini wachezaji bora wa USM Alger na kuwapa mbinu wachezaji wake namna ya kukabiliana nao.

"Niwapongeze wachezaji wangu wamepambana na kufanikiwa kufika fainali ya michuano hii ya CAF, kazi iliyobaki kwetu ni kuhakikisha tunafanya vizuri kwenye hatua hii, kuna mbinu ambazo tunazifanyia kazi na kuwapa wachezaji wetu, tunaamini tutafanya vizuri," alisema Nabi.

Alisema pia anashukuru viongozi wa Yanga kwa kushirikiana naye bega kwa bega kuanzia mwanzo wa msimu kwa kufanya usajili mzuri na kuhakikisha wanapata mahitaji yote.

Nabi anasema tayari amewaambia wachezaji wake kuwa ni lazima wamalize kazi kwenye mchezo wao wa nyumbani ili kujiweka katika mazingira mazuri kuelekea kwenye mchezo wa marudiano.

Alisema wamegundua mbinu wanazozitumia wapinzani wao kwenye michezo ya ugenini na ile wanayotumia kwenye michezo wanayokuwa nyumbani.

"Jambo kubwa ambalo kama benchi la ufundi tunalifanyia kazi kwa umuhimu mkubwa ni kutafuta namna ya kuhakikisha

INAENDELEA UK. 23

# Fedha za Super League zaipa kiburi Simba

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa klabu ya Simba umesema una uwezo wa kufanya usajili wa mchezaji yeyote wanayemtaka kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao kwa kuwa fedha za kufanya hivyo wanazo.

Simba inatarajia kupata fedha zaidi ya Sh. bilioni tano kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF) za maandalizi ya michuano ya Super League lakini kuna fedha watakazozipata kutokana na kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu kiasi cha Dola za Marekani 900,000 ( zaidi ya Sh. bilioni 2.1).

Kwa mujibu wa habari kutoka ndani ya klabu hiyo, zinasema uongozi wa timu hiyo utatumia sehemu kubwa ya fedha hizo kukiboresha kikosi chao kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu.

Simba tayari imeanza kuhusishwa na majina ya nyota mbalimbali wa ndani na nje ya nchi.

Moja ya majina ya wachezaji wa ndani wanaohusishwa kujiunga na Simba ni kiungo nyota wa Azam FC, Sospeter Bajana.

Bajana amehusishwa kujiunga na Simba baada ya mkataba wake na Azam FC kufikia ukingoni huku ikidaiwa kuwa hajaongeza mkataba na waajiri wake hao ambao wako katika mazungumzo.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema uongozi wa timu hiyo unaendesha mchakato wao wa usajili kwa umakini mkubwa.

"Bado hatujaweka wazi wachezaji tunaowataka ingawa yapo majina ya wachezaji tunaowataka, uongozi upo makini kufanya usajili wa nguvu kwa sababu fedha zipo," alisema Ahmed na kuongezea,

"Tuna mzigo mkubwa ukiunganisha fedha za mwekezaji wetu, Mohammed Dewji, fedha za Super League na vyanzo vingine, hii itatufanya kuwa na jeuri ya kufanya usajili kwa wachezaji tunaowataka," alisema.

Kuhusu kumtaka kiungo wa Azam FC, Bajana, Ahmed alisema

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >